PROTOTYPE

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

# KISWAHILI LANGUAGE

## TEACHER'S GUIDE



SENIOR ONE

LOWER SECONDARY CURRICULUM

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

# KISWAHILI LANGUAGE

# TEACHER'S GUIDE

## SENIOR ONE

LOWER SECONDARY CURRICULUM

NCDC
NATIONAL CURRICULUM
DEVELOPMENT CENTRE

Published 2020

This material has been developed as a prototype for implementation of the revised Lower Secondary Curriculum and as a support for other textbook development interests.

This document is restricted from being reproduced for any commercial gains.

National Curriculum Development Centre
P.O. Box 7002,
Kampala- Uganda
www.ncdc.co.ug

# YALIYOMO

DIBAJI ........................................ iv

SHUKURANI ........................................ v

MUHULA WA KWANZA ........................................ 1

MADA KUU 1.1: WATU WA NYUMBANI ........................................ 1

MADA KUU 1.2 JAMII ........................................ 18

MADA KUU 1.3 HESABU ........................................ 36

MUHULA WA PILI ........................................ 52

MADA KUU 1.4 WANYAMA NA NDEGE ........................................ 52

MADA KUU 1.5 MIMEA NA MATUNDA ........................................ 66

MADA KUU 1.6: BIASHARA ........................................ 81

MUHULA WA TATU ........................................ 90

MADA KUU: 1.7 NYUMBA ........................................ 90

MADA KUU 1.8 SHULENI ........................................ 101

MADA KUU 1.9: MICHEZO ........................................ 112

# DIBAJI

Mwongozo huu umetayarishwa kumwezesha mwalimu kufasiri mtalaa mpya uliorekebishwa. Pia utamwezesha kutumia kitabu cha wanafunzi vizuri. Mwongozo wa mwalimu humshauri mwalimu kuhusu kile anachostahili kufanya wakati na baada ya kufundisha.

Ili kurahisisha kazi ya mwalimu, shughuli zote na maagizo ya maswali yaliyomo katika kitabu cha mwanafunzi yamejumlishwa katika mwongozo huu ila kuna taarifa nyingine na majibu pendekezwa ambayo yameongezwa.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia lengo kuu la mtalaa uliorekebishwa unaoangazia umilisi wa mwanafunzi unaohitajika katika karne ya 21, huku ukikuza maadili, mitazamo, na milisi zake katika masomo ili kumtayarisha mwanafunzi kuendelea na masomo na mwisho kupata kazi.



**Profesa Mshiriki Betty Ezati**
Chairperson, NCDC Governing Council

# SHUKURANI

Kituo cha Taifa cha Kuendeleza Mtalaa (NCDC) kinashukuru wote walioshiriki katika kuandika mwongozo huu.

Tunashukuru taasisi zote ambazo zilitupa walimu walioshiriki katika kuandika mwongozo kama paneli. TunaMshukuru Galacha wa Kiswahili ambaye alianzisha kazi hii ya kutayarisha mwongozo ambao utamfaa mwalimu katika ufundishaji wake. Shukurani zetu za dhati ziwafikie watu wa shirika la **Enabel** ambao walitupa ushauri wa kitaaluma wakati wa kuandika mwongozo huu.

Kituo cha NCDC kinashukuru sana walimu na wanafunzi ambao walishirikiana na Galacha na Wataalamu kutoka Cambridge Education and Curriculum Foundation ili kutuwezesha kutoa mwongozo huu.

NCDC ingependa kuwashukuru wale wote ambao hawakujitokeza moja kwa moja kushiriki katika uandishi wa mwongozo huubali walikuwa nyuma ya pazia wakichangia kwa njia moja au nyingine.

NCDC inahakikisha kuwa itatunza kanuni na maadili yaongozayo uandishi wa vitabu. Katika uandishi wa kitabu hiki, asilia mbalimbali zimerejelewa ambazo hatuwezi kushukuru vya kutosha tukazimaliza. Asanteni nyote.

Natoa wito kwamba mapendekezo yoyote kuhusu uboreshaji wa huduma zetu yanakaribishwa. Tafadhali tufikie kupitia kwa sanduku la posta, 7002, Kampala au kwa anwani pepe: admin@ncdc.go.ug

**Grace K. Baguma**
Mukurugenzi, National Curriculum Development Centre

# MUHULA WA KWANZA

# MADA KUU 1.1: WATU WA NYUMBANI





**Misamiati Msingi**
ukoo
salamu
adabu
uakifishaji

**Umilisi**

Mada hii itakuwezesha;

- Kutamka sauti za Kiswahili kwa usahihi
- kutambua misamiati ya watu wa nyumbani.
- kusimulia hadithi fupi kuhusu familia yako.
- kuanzisha na kuitikia salamu kwa namna inayostahili.
- kutambua na kuigiza maneno ya adabu
- kusoma na kuigiza mazungumzo.
- kutambua na kutumia aina mbalimbali ya majina ya watu wa nyumbani katika sentensi.
- kubaini vipatanishi vya nomino vya ngeli ya A–WA katika sentensi.
- kuakifisha nomino katika sentensi kwa kuzingatia alama zote za uakifishaji.
- kutambua hatua mwafaka za kuandika insha ya mwongozo.
- kuandika insha ya mwongozo.

**Utangulizi**

Katika mada hii, mwanafunzi aweze kutambua watu anaoishi nao nyumbani, kutamka majina yao kwa ufasaha, kutambua silabi katika maneno au majina mbalimbali, na kuwasiliana kwa ufasaha. Mwanafunzi pia, aweze kutambua umuhimu wa kuthamini na kushirikiana na watu wa nyumbani kimazungumzo na katika shughuli mbalimbali.

Kwa hivyo, mada hii itampa mwanafunzi uwezo wa kutambua matamshi bora ya sauti za Kiswahili pamoja na kumwezesha kutambua watu wa nyumbani na jinsi ya kuwasiliana na kuishi nao kwa namna inayostahili.

**Maandalizi pendekezwa ya mwalimu**
Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Kanda za sauti
- Kadi zenye maadishi ya sauti mbalimbali za Kiswahili
- Chati
- Michoro/picha
- Kanda za video
- Projekta
- Kamusi

**Funzo a: Kutamka sauti za Kiswahili**
**Shughuli 1.1 Kusikiliza na Kuzungumza**

Katika funzo hili, wanafunzi watajifunza kuhusu sauti za Kiswahili. Tamka kila vokali kwa usahihi ukihakikisha kila mwanafunzi anakusikiliza kwa makini. Waongoze katika makundi yao, kutamka, kukariri, na kusoma vokali kwa sauti. Tembelea kila kikundi ukihakikisha kila mwanafunzi anatamka vokali kwa ufasaha.

Waongoze wanafunzi, kutamka vokali na kisha baadhi ya maneno yenye sauti hizo.
Kwa mfano;
a- anza, baba, kaka, dada
**e**- endesha, endelea,
**i**.inuka, ingia, bibi, mimi, sisi
**o**- omba, ona, ondoa, oga, wote
**u**- uhuru, umoja, kuku, nguvu

Waongoze wanafunzi, kutamka baadhi ya maneno yenye vokali mbili zinazofanana.
Kwa mfano;

**aa**- kaa, jaa, baada, saa,
**ee**- mzee, pekee
**ii**- tii, bidii
**oo**- choo, njoo

**uu**- juu, mguu

Waongoze wanafunzi, kutamka baadhi ya maneno yenye vokali zisizofanana ambazo hufuatana.
Kwa mfano;

ondoa, lia, ongea, fagia, pokea, chuo, kimbia, somea

1. Waongoze wanafunzi kutamka na kuandika baadhi ya maneno yenye vokali mbalimbali.
2. Hakikisha kila mwanafunzi ametamka maneno kwa usahihi.

**Shughuli 2.1 Kusikiliza na Kuzungumza**

1. Wanafunzi wakiendelea kujifunza sauti za Kiswahili, tamka kila konsonanti kwa usahihi. Hakikisha kila mwanafunzi anakusikiliza kwa makini. Waongoze katika makundi yao, kutamka, kukariri, na kusoma konsonanti kwa sauti. Tembelea kila kikundi ukihakikisha kila mwanafunzi anatamka konsonanti kwa ufasaha.
2. Waongoze wanafunzi kutambua mahali ambapo konsonanti hizi zinatamkiwa na namna zinavyotamkwa.

i. /b/, /p/, /m/ /w/

ii. /f/, /v/

iii. /dh/, /th/

iv. /d/, /l/, /n/, /r/, /s/, /t/, /z/

v. /ch/, /j/, /ny/, /sh/, /y/

vi. /k/, /g/, /ng'/, /gh/, /kh/

vii. /h/.

1. Waongoze wanafunzi katika vikundi vyao kutambua na kuandika alfabeti ya Kiswahili kutoka **A** hadi **Z**
2. Waongoze wanafunzi kuunganisha konsonanti na vokali walizotamka hapo juu ili kuunda silabi na maneno. Kwa mfano; ba, be, bi, bo, bu – baba, beba, bubu nk

## Funzo b.  Kutambua msamiati wa watu wa nyumbani

### Shughuli 3.1 Kusikiliza na kuzungumza

1. Waongoze wanafunzi kutambua na kutaja watu wanaoishi nao nyumbani kv, baba, mama, kaka, shangazi nk
2. Washirikishe wanafunzi kutafuta maana ya maneno waliyopewa katika boksi kwa mfano katika matumizi ya kamusi au ukiwaongoza wewe mwenyewe.

| |
|---|
| baba, mama, kaka, dada, bin, binti, shangazi, babu, nyanya |

3. Waeleze wataje majina ya watu wanaoishi nao katika familia zao.
4. Washirikishe wanafunzi kusoma wakijadiliana maana ya sentensi zifuatazo

i. Baba yangu ni dereva wa basi.
ii. Mama yangu ni mwalimu wa Kiswahili.
iii. Dada yake Peter anafundisha katika Chuo Kikuu cha Kyambogo.
iv. Bin yangu anaitwa Haba.
v. Kaka yangu anasomea katika Chuo cha walimu cha Nakaseke.
vi. Binti yake Yusuph ni mrembo sana.
vii. Tafadhali niitie yule kaka yangu.
viii. Eve ni binti yake mzee Lutaaya.
ix. Dada yako anaitwa nani?
x. Mama ananyonyesha mtoto.

**Kazi mradi**

Wagawe wanafunzi katika kikundi. Wape mradi wa kutafuta maneno au msamiati mwengine unaohusiana na ukoo. Waelekeze jinsi ya kutumia kamusi kutambua msamiati huo. Wape muda wa karibu sana kuwasilisha darasani matokeo yao.

5. Waelekeze wanafunzi kutmbua na kuambatanisha majina ya ukoo kutoka sehemu **A** na **B.**

| A | B |
|---|---|
| (a) Mama | ni mtoto wa shangazi, ami au mjomba. |
| (b) Babu | ni ndugu wa kike wa baba, au ni ndugu wa kike wa kuumeni. |
| (c) Shangazi | ni mzazi wa kike. |
| (d) Ami | ni mwanamume aliyezaliwa katika tumbo moja na baba. |
| (e) Binamu | ni mzazi wa kiume wa baba au mama. |


**Funzo c: Kuigiza majukumu ya watu wa Nyumbani**

**Shughuli 4.1 Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na Kuandika**

1. Washirikishe wanafunzi kutazama michoro. Wape nafasi kuzungumzia wanachoona.


a


b

c


d



e

f


2. Waongoze wanafunzi kuambatanisha sentensi zilizo katika boksi na michoro uliyotazama hapo juu

| | |
|---|---|
| Bibi anasuka mkeka | Dada anafagia |
| Watoto wanaruka kamba | Baba anakama ng'ombe |
| Mama anapika | Shangazi analima |

3. Washirikishe wanafunzi katika vikundi kuelezea na kuigiza majukumu mbalimbali ya watu wa nyumbani.

**Funzo d. Kueleza kazi zinazofanyika nyumbani**

**Shughuli 5.1 Kusikiliza, kuzungumza na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu kazi mbalimbali zinazofanyika nyumbani kwao.
2. Waongoze katika zamu mmoja baada ya mwingine kuelezea kazi anazofanya nyumbani kwao wakati wa likizo.
3. Washirikishe katika makundi yao, kujaza na kukamilisha sentensi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo vinavyohusu kazi za nyumbani.

(paka, ezeka, jenga, safisha, fyeka)

(a) Dada yangu ana …… safisha ………….. vyombo.
(b) Ami ali ……… fyeka ……….. nyasi katika ua la boma lake.
(c) Baba yetu anafanya kazi ya ku …… paka, …… rangi.
(d) Nili … ezeka ……… mabati juu ya nyumba yetu.
(e) Babu yetu ali …… jenga ……. nyumba kubwa sana kijijini.

**Funzo e. Kusimulia hadithi fupi kuhusu familia**


**Shughuli 6.1 Kusikiliza, kuzungumza na Kuandika**

Waelekeze wanafunzi kuchora watu wanaoishi nao nyumbani kwenye karatasi, na kisha washirikishe kusimulia hadithi inayohusu watu wa familia yake.

**Funzo f. Kutambua matumizi ya Salamu na maneno ya adabu**

**Shughuli 7.1 Kusikiliza na kuzungumza**

Washirikishe wanafunzi kutazama na kutaja kuhusu chochote wanachoona katika michoro. Washirikishe tena kuelezea na kuigiza kile kinachotendeka katika mchoro.




***Taz:*** Salamu ni maamkizi ya kujuliana hali miongoni mwa watu. Katika lugha ya Kiswahili kuna aina nyingi za salamu kulingana na umri/cheo, wakati, hali, idadi ya watu unaosalimia na uhusiano wa watu husika.

1. Waweke wanafunzi katika makundi ya jozi, washirikishe kusalimiana na wenzao kwa kutumia salamu zifuatazo;

| **Salamu** | **Jibu** |
|---|---|
| Shikamoo | Marahaba |
| Shikamoo baba? | Marahaba mwanangu |
| Shikamoo mama? | Marahaba mwanangu |
| Shikamoo mwalimu? | Marahaba |
| Shikamoo shangazi? | marahaba |
| Shikamoo babu? | Marahaba mjukuu wangu |
| Shikamoo bibi/nyanya? | Marahaba mjukuu wangu |


**Tanbihi:** Shikamoo ni salamu ya heshima kwa mtu anayekuzidi umri au cheo.

**i. Salamu kulingana na wakati.**

| **Salamu** | **Jibu** |
|---|---|
| Sabalkheri | Sabalkheri/Alkheri |
| Masalkheri | Masalkheri/Alkheri |




Sabalkheri ni salamu inayotumiwa wakati wa asubuhi ilhali masalkheri inatumiwa wakati wa jioni kuanzia alasiri.



**ii. Salamu kulingana na hali mbalimbali**

| Salamu | Hali | Jibu |
|---|---|---|
| Habari ya/za | Masomo/Shuleni? | Nzuri /njema |
| Habari ya/za | Nyumbani? | Nzuri /njema |
| Habari ya/za | Safari? | Nzuri /njema |
| Habari ya/za | Kupotea? | Nzuri /njema |
| Habari ya/za | Kazi? | Nzuri /njema |








**iii. Salamu za kujuliana hali kulingana na idadi ya wanaoitikia.**

**Shughuli 8.1 Kusikiliza na kuzungumza**

Waongoze wanafunzi kuigiza salamu na majibu yake kama ifuatavyo;

| Salamu | Jibu |
|---|---|
| Hujambo? | Sijambo |
| Hamjambo? | Hatujambo |
| Umeamkaje? Umelalaje? | Salama |
| Mmeamkaje? Mmelalaje? | Salama |
| Umeshindaje? Mmeshindaje? | Vizuri/vyema |
| U mzima? M wazima? | Ni mzima/ Tu wazima |
| Uhali gani? Mhali gani? | Njema/ Nzuri |




**Funzo g. Kutambua na kuigiza maneno ya adabu**
**Shughuli 9.1 Kusikiliza, kuzungumza na kusoma**

Washirikishe katika makundi yao, kusoma na kuigiza maneno ya adabu yafuatayo;

| Neno la adabu | Jibu |
|---|---|
| Hodi hodi! | Karibu! |
| Karibu | Asante |
| Kwa heri | Kwa heri ya kuonana |
| Hongera | Asante |
| Asante kwa kazi | Karibu |
| Pole | Haidhuru/ Nimeshapoa |

**Funzo h. Kusoma na kuigiza mazungumzo**
**Shughuli 10.1 Kusoma na kuandika**

1. Katika jozi, waongoze wanafunzi kusoma na kuigiza mazungumzo yafuatayo kisha washirikishe kujibu maswali

**Tom** : Habari ya siku nyingi rafiki?
**Rehema** : Ni nzuri, labda zako?
**Tom** : Mimi ni mzima. Umepotea sana siku hizi!
**Rehema** : Ndiyo, mama yangu amekuwa mgonjwa.
**Tom** : Eee! Pole sana, sasa yuko vipi?
**Rehema** : Tumempa dawa, atapata nafuu.
**Tom** : Hebu tuombe Mungu apone haraka
**Rehema** : Amina. Hebu niende nyumbani, Alamsiki!

i. Washirikishe katika makundi yao, kutambua maneno mapya kutokana na mazungumzo na kisha kutafuta maana ya maneno hayo mapya.

ii. Washirikishi kutambua na kuandika salamu na maneno ya adabu yaliyotumika katika mazungumzo.kwa mfano; Habari ya siku nyingi? nk

**<u>Sarufi</u>**


**<u>Funzo i.</u> Kutumia vipatanishi sahihi vya nomino za ngeli ya A-WA katika sentensi**

**Shughuli 11.1 Kusoma na kuandika**

1. Waelekeze wanafunzi kutazama na kuzungumzia kuhusu kinachotendeka katika michoro.

**Umoja** **Wingi**













2. Waongoze kuambatanisha sentensi kutoka boksi na michoro waliyotazama hapo juu.

| | |
|---|---|
| Mtoto analia | Watoto wanalia |
| Mkulima analima | Wakulima wanalima |
| Msichana anafagia | Wasichana wanafagia |

3. Washirikishe wanafunzi kusoma kwa sauti na kutafuta maana ya nomino zifuatazo. Waongoza wanafunzi kuhusu jinsi ya kutumia kamusi kutafuta na kuelezea maana ya maneno mbalimbali.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mtu | Watu |
| Mtoto | Watoto |
| Mwalimu | Walimu |
| Mkulima | Wakulima |
| Mzazi | Wazazi |
| Mke | Wake |
| Mume | Waume |
| Mgeni | Wageni |
| Mfalme | Wafalme |
| Mwanafunzi | Wanafunzi |
| Mhubiri | Wahubiri |
| Mvulana | Wavulana |
| Msichana | Wasichana |
| Mganga | Waganga |
| Mchezaji | Wachezaji |
| Mshonaji | Washonaji |
| Mlevi | Walevi |
| Mlinzi | Walinzi |
| Mwislamu | Waislamu |
| Mgonjwa | Wagonjwa |

**Taz;** Ngeli ya a-wa inajumuisha vitu kama, watu, wanyama, wadudu, ndege na kadhalika.

4. Waongoze wanafunzi katika makundi yao kufanya utafiti katika kamusi, maktaba au mtandaoni kuhusu nomino nyingine za ngeli ya **a-wa** na uziandike kwa umoja na wingi

5. Washirikishe kwa kujadiliana na wenzao kuandika sentensi zifuatazo katika wingi. Kwa mfano;

i. Mama analima shambani. – Kina mama wanaima mashambani
ii. Kaka na dada wanaosha vyombo. – Kaka na dada wanaosha vyombo.
iii. Mfalme amekaa. – Wafalme wamekaa
iv. Mganga anatibu mgonjwa. – Waganga wanatibu wagonjwa
v. Mvulana anapasua kuni. - Wavulana wanapasua kuni.
vi. Mzee anapeana mawaidha. – Wazee wanapeana mawaidha.
vii. Mwanafunzi aliendа shuleni asubuhi. – Wanafunzi walienda shuleni asubuhi.

**Funzo j. Kuakifisha kwa usahihi**
**Shughuli 12. 1 Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi kusoma na kujadili ujumbe katika kifungu.

Nalubega na Onyango ni marafiki sana. Siku moja, Nilimsikia Onyango akisema, "Mimi na rafiki yangu Nalubega tumetembelea mataifa mengi ulimwenguni." Kwa mfano, Mataifa ya Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania, Sudani Kusini, Rwanda na Burundi), Ujerumani, Uhispania, Brazil, Marekani na Uchina. "Umetembelea nchi gani wewe?" Aliniuliza. "Mimi sijawahi hata kuvuka mpaka wa Uganda!" Nilimjibu. Alaa! Alishangaa. Bahati yako itakuja usijali. Alinitia moyo.

1. Waelekeze wanafunzi kutambua na kuandika alama za uakifishaji katika kifungu wanalichosoma.
2. Waelekeze wanafunzi kufanya utafiti kuhusu alama nyingine zozote za uakifishaji ambazo hazijatajwa katika kifungu.

**Funzo K. Kuandika Insha**

**Shughuli 13.1 Kuandika**

1. Washirikishe kila mwanafunzi kujadiliana na kuandika insha kuhusu watu wa ukoo wake. Waelekeze kuhusu jinsi ya kuzingatia mwongozo uliopewa wa kuandika insha. Kwa mfano; mwanafunzi katika maandishi ajitambulishe, Kidato anachosoma, anakoishi, watu anaoishi nao nyumbani, kwao, aelezee kuhusu kazi zao wanazofanya, na jinsi yeye mwenyewe anavyosaidia wazazi wake katika kazi za nyumbani.

**Zingatia**

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. Woongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi.

Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli Jumlishi**

Umeandaliwa sherehe ya siku ya kuzaliwa kwako nyumbani kwenu. Umeita baadhi ya marafiki zako kutoka darasani mwako kuhudhuria. Baada ya chakula na kukata keki, umeombwa kutambulisha kila mtu aliyehudhuria. Umemaliza kuwatambulisha marafiki zako.

a. Watambulishe watu wa ukoo wako waliohudhuria.
b. Kila mtu wa nyumbani alisema kuwa marafiki zako ni watoto wenye adabu. Ni mambo gani waliyofanya ili kuonyesha kuwa ni wenye adabu.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu;*

- Sauti za Kiswahili kwa usahihi
- Msamiati wa watu wa nyumbani.
- Usimulizi w hadithi fupi kuhusu familia yako.
- Salamu kwa namna inayostahili.
- Maneno ya adabu
- Uigizaji wa mazungumzo.
- Matumizi ya aina mbalimbali ya majina ya watu wa nyumbani katika sentensi.
- Vipatanishi vya nomino vya ngeli ya A–WA katika sentensi.

- Uakifishaji.
- Uandishi wa insha

Kuhusu Shughuli jumlishi iliyo juu, utatumia jedwali la kupimia umilisi wa mwanafunzi. Umilisi wa kila mwanafunzi utapimwa kulingana na kila kipengele cha tathmini kilichomo katika shughuli jumlishi. Kwa mfano, mwanafunzi ambaye atapata alama 2/3 au zaidi kutokana na (3) ambazo zinatarajiwa, huyo atachukuliwa kuwa amepata umilisi lengwa. Yule ambaye atapata alama ya chini, atastahili kuongozwa tena katika kufanya marudio na marekebisho kwa kurejelea vipengele vya mada ambavyo hajaelewa ili apate umilisi lengwa.

| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1. **Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| 1. Watambulishe watu wa ukoo wake waliohudhuria. | - Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja majina ya ukoo wake angalau 7 na kuendelea, mpe 3/3.<br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja majina ya ukoo wake angalau 5-6, mpe 2/3.<br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja majina ya ukoo wake angalau 3-4, mpe 1/3.<br><br>-Mwanafunzi atakayepata alama chini ya mbili aongozwe | Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja majina ya ukoo wake katika maelezo na jinsi yanavyoambatana kiutaratibu.<br><br>-Kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Kwa kiwango cha wastani mpe 2/3.<br><br>- Kwa kiwango cha chini, mpe 1/3. | Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja majina ya ukoo wake katika maelezo kwa kuzingatia sarufi sahihi, alama za uakifishaji, upatanisho wa ngeli ya a-wa kwa uhakika.<br><br>-Aliye kwenye kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Aliye kwenye kiwango cha wastani mpe 2/3.<br>- Aliye kwenye kiwango cha | Mwanafunzi ambaye ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |

| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1**.** **Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| | kurudia kazi ili kupata umilisi lengwa. | | chini, mpe 1/3. | |
| 1. Mambo yanayomfanya mtu kuwa mwenye adabu, | - Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja maneno pamoja na vitendo vya adabu angalau 8, mpe 3/3.<br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja maneno pamoja na vitendo vya adabu angalau 6, mpe 2/3.<br><br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja maneno pamoja na vitendo vya adabu angalau 3-4, mpe 1/3.. | - Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja maneno pamoja na vitendo vya adabu kwa utaratibu na muumaano mzuri wa maelezo au maadishi,<br><br>Aliye kwenye kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha Aliye kwenye kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha chini mpe 1/3 | Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja maneno ya adabu au kuigiza vitendo sahihi vya maneno ya adabu, matumizi mazuri ya sarufi, alama za uakifishaji, upatanisho wa ngeli ya a-wa kwa usahihi;<br><br>-Aliye tumia haya kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Aliye kwenye kiwango cha wastani mpe 2/3.<br>- Aliye kwenye kiwango cha chini, mpe 1/3. | Mwanafunzi ambaye ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |

Baada ya kutambua kiwango cha umilisi wa mwanafunzi wako, utaunganisha na kujumlisha alama aliyopata kutokana na uwiano, muumano, uhakika pamoja na ile alama ambayo atapata iwapo atakuwa amepitisha au kuongeza majibu ambayo hayakuwa matarajio yako. Baada ya kuzijumlisha, utaziandika juu ya alama tarajiwa zote kwa jumla na kisha uzidishe tatu. I wapo vipengele ni vingi, utafanya kama hapo juu na kisha utaunganisha alama za vipengele vya tathmini na mbalimbali ambavyo viko katika shughuli jumlishi na kisha jumla yake kuiandika kiwastani.

Alama ya mwisho utakayopata, ndiyo utahifadhi katika rekodi ya kumbukumbu ya tathmini ya wanafunzi.

# MADA KUU 1.2 JAMII



**Msamiati Msingi**
dira
mazingira
sudi
dhehebu
kiama
jahanam

**Umilisi**

Mada hii itakuwezesha;

a. kutambua msamiati wa mahali muhimu.
b. kutofautisha na kubaini sehemu za dira.
c. kujadili shughuli zinazofanyika katika mahali muhimu.
d. kuelezea sehemu muhimu mbalimbali kwa kutumia dira.
e. kusomea makala na kujibu maswali.
f. kutambua na kutumia vitenzi mbalimbali katika sentensi.
g. kubaini matumizi ya vipatanishi vya nomino katika sentensi vya ngeli ya U–I.
h. kubaini na kutumia alama zote za uakifishaji katika sentensi na vifungu vya maneno.
i. kutambua vipengele muhimu vya uandishi wa insha ya mwongozo.
j. kuandika insha ya mwongozo.

**Utangulizi**

Katika mada hii, mwanafunzi aweze kutambua kuwa ni wajibu wake kujua yanayotendeka katika jamii yake. Pia, anastahili kujua mahali muhimu katika mazingira yake, huduma mbalimbali zinazopatikana katika mahali muhimu. Awe na uwezo wa kumwelekeza yeyote anayekwenda katika mahali muhimu kokote bila kupoteza njia. Aweze kutambua jinsi jinsi ya kuchangia katika kuhifadhi na kuendeleza mahali muhimu katika jamii yake. Kwa hivyo, mada hii, itamwezesha mwanafunzi kutambua na kutumia msamiati unaohusiana na mahali muhimu, matumizi ya dira pamoja na vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika mawasiliano.

**Maandalizi pendekezwa ya mwalimu**
Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Kanda za sauti
- Kadi zenye maadishi ya sauti mbalimbali za Kiswahili
- Chati
- Michoro/picha
- Kanda za video
- Projekta
- Kamusi

**Funzo a. Kutambua msamiati wa mahali muhimu katika Jamii**

**Shughuli 1.2 Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi kushirikiana kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa katika makala hii.

Jamii yetu huwa ikijumuisha sehemu mbalimbali ambazo zina umuhimu mkubwa sana katika maisha ya mwanadamu. Bila sehemu hizi, maisha ya mtu hayawezi kuboreka hata kamwe kwa sababu atapatwa na upungufu fulani. Hizi ni sehemu ambazo tangu jadi zimekuwepo na michango yake haiwezi ikapigiwa mifano.

Mojawapo ya sehemu hizi maalum katika jamii ni kituo cha polisi. Hili ni jengo lililojengwa kwa kusudi la kuimarisha amani katika jamii. Iwapo mtu yeyote anavunja sheria basi hupelekwa katika kituo cha polisi ili akafunguliwe mashtaka na baadaye afikishwa mahakamani kukatiwa hukumu yake. Kutokana na kuwepo kwa kituo cha polisi katika jamii, visa vibaya vya uhalifu vimeepukwa kwa viwango vikubwa.




Vile vile, kuna sehemu za kuabudia katika jamii ambapo Wakristo huenda kanisani kila Jumamosi au Jumapili kulingana na dhehebu la mwuumini husika. Nao Waislamu vile vile, huelekea misikitini kuabudu. Kwa siku angalau wao huabudu mara tano. Siku ya Ijumaa ndiyo siku rasmi ya ibada katika dini ya Kiislamu. Maeneo haya ya ibada yamekuwa na mchango mkubwa sana katika uelekezi wa sudi za wanadamu. Watu wamefunzwa kumcha Mungu na kuwaheshimu wenzao ili duniani kuwe na amani. Vile vile, ni katika majengo haya ya ibada ambapo waumini hufunzwa kuishi maisha mema na kujiepusha na dhambi ili siku ya kiama wasielekee jahanamu kuchomwa moto wa milele.





Shule nayo ni mahali ambapo elimu hupokezwa kwa wanafunzi ili waweze kuwa na maarifa ya kuwaongoza katika maisha yao siku za baadaye. Kuna shule za chekechea, msingi, upili na taasisi za juu za elimu kama vile vyuo vya ufundi na vyuo vikuu. Taifa letu limeweza kupiga hatua mbele kimaendeleo kwa sababu watu wengi wameweza kupokea elimu kutoka katika mashule mbalimbali.



Mahakama ni mahali ambapo hukumu hutolewa kwa wale wanaovunja sheria. Hili ni eneo ambalo limesaidia sana katika kudumisha uungwana ndani ya jamii yetu. Wanaopatwa na hatia huwa wakipewa adhabu kulingana na makosa waliyoyafanya. Kwa mfano, kuna wale ambao huwa wakihukumiwa kifungo cha miezi hadi kufikia wale wanaohukumiwa kifungo cha maisha gerezani.



Hatimaye, hospitali na zahanati nazo zimekuwa na wajibu mkubwa sana katika maisha ya wanadamu kwa sababu ya kuwahudumia wale wote ambao ni wagonjwa. Matibabu mbalimbali yemekuwa yakitolewa kwa wagonjwa wa aina tofauti tofauti hospitalini bila kujali umri, rangi wala jinsia ya mgonjwa. Hili limewaepusha wagonjwa wengi kufariki kutokana na maradhi ambayo yamekuwa yakiwakumba kila siku.



1. Washirikishe wanafunzi katika makundi yao kutafuta maneno mapya kutokana na makala hii, kisha waongoze kutumia kamusi au mtandao wa intaneti kuelezea maana ya maneno mapya hayo.
2. Waongoze wanafunzi kwa kuandika mahali muhimu katika jamii zao.
3. Washirikishe wanafunzi kukamilisha sentensi mbalimbali.

i. Taja sehemu ambayo wanafunzi hupewa elimu
……………shuleni……………..……………..
ii. Mahali ambapo watu huenda kuabudia huitwaje? ………..kanisa au msikiti………..…………………….
iii. Ni mahali papi ambapo wahalifu hupekelwa ili wahukumiwe?
………..mahakamani……………….
iv. Kituo cha polisi kina manufaa gani? ………..maaskali polisi hukaa hapo wanaolinda Amani na usalama………………………………………….
v. Wagonjwa hutibiwa mahali papi?
……hospitalini…………………………………………………

**Funzo b: Kueleza umuhimu wa sehemu muhimu katika jamii**
**Shughuli 2.2: Kusikiliza na kuzungumza**

Waongoze wanafunzi kutambua na kuandika mahali muhimu katika mazingira yao, kisha waelekeze waeleze kuhusu umuhimu wa kila mahali muhimu.

**Funzo c. Kujadili shughuli zinazofanyika katika mahali muhimu**
**Shughuli 3.2: Kuzungumza na kuandika**

1. Washirikishe wanafunzi kujadili mahali muhimu mbalimbali katika jamii. Kama vile kanisa, msikiti, hospitali nk
2. Waelekeze kujadiliana kuhusu shughuli zinzaofanyika katika mahali muhimu.
3. Waongoze wanafunzi kuandika shughuli hizo na kutunga angalau sentensi mbili kwa kila shughuli.

**Funzo d. Kutambua sehemu za dira**
**Shughuli 4.2: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi kuchora sehemu za dira
2. Washirikishe kuonyesha sehemu zote za dira
3. Waelekeze kila mmoja kuelekeza upande wa nyumbani kwake kutoka mahali muhimu mbalimbali.
4. Washirikishe kuandika angalau wilaya mbili kutoka pande nne za nchi ya Uganda.

**Taz:** Dira ni kifaa kinachoonyesha pande za dunia ambacho huwaongoza watu kutambua maeneo mbalimbali. Mielekeo hii humwongoza mtu ajue kule anakolenga kwenda. Mfano ni Kaskazini, Kusini, Katikati, Magharibi na Mashariki. Hii ndiyo mielekeo mikuu ya dira. Pia kuna ile mielekeo midogo ya dira kama Kaskazini mashariki, Kaskazini magharibi, Kusini mashariki na Kusini magharibi. Mwongozo huu wa mielekeo ya pembe za ulimwengu ni muhimu sana kila mtu kuielewa.

**Funzo e: Kueleza sehemu muhimu katika jamii kwa kutumia dira.**
**Shughuli 5.2 Kusikiliza na kuzungumza**

Waweke wanafunzi katika katika makundi na uwaongoze kusoma na kuigiza mazungumzo haya kisha waelekeze kubadilishana mawazo na majukumu.



**Okecho:** Samahani Anyango. Je, unaweza nionyesha barabara inayoelekea benkini?

**Anyango**: Naam, bila shaka. Pinduka kushoto mwishoni mwa barabara hii.

**Okecho:** Karibu na taa zinazoelekeza watu na magari barabarani?

**Anyango**: Ndio. Kisha nenda hadi ufike kwenye mzunguko wa barabara hii.

**Okecho**: Je, baada ya mzunguko huo nifanyeje?

**Anyango:** Upinde mkono wa kulia wa mzunguko huo na ujiunge na barabara ya Maji Matulivu.

**Okecho:** Ni sawa. Nifikapo pale nitakuwa nimewasili?

**Anyango:** La, fuata barabara hiyo ya Maji Matulivu na benki utaiona kwa upande wa kushoto wa barabara ile.
**Okecho:** Asante sana dada.

**Anyango:** Kwa heri.

1. Waelekeze kutafuta maneno mapya kutokana na mazungumzo, kisha waongoze kutumia kamusi kuelezea maana ya maneno hayo.
2. Washirikishe kuelekezana jinsi wenzao wanavyoweza kuwatembelea nyumbani kweo.

**Funzo f: Kusoma makala kuhusu mahali muhimu na mtumizi ya dira.**

**Shughuli 6.2 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, wahirikishe kusoma na kujadili taarifa kutokana na makala hii.

**NAPENDA JAMII YETU**

Katika jamii yetu, watu wanaishi vizuri na kwa amani. Watu katika jamii hii hufanya kazi kwa bidi na kutunza mazingira yao kwa unadhifu.

Kuna mahali muhimu katika jamii yetu. Mahali huku hutusaidia sote wanajamii. Kwa mfano, kuna hospitali mbili katika jamii yetu. Hospitali moja inaitwa Kitagata na ya pili inaitwa Kabwohe. Hospitali hizi zinatusaidia sana. Wagonjwa, wanawake wajawazito na wengine wanaohitaji msaada hukimbilia hospitali hizi. Madaktari na manesi katika hospitali hizi huhudumia watu vizuri sana. Pamoja na hospitali, kuna kanisa na misikiti. Kanisa na misikiti ni mahali muhimu katika jamii yetu. Husaidia kufariji watu na kuwapa imani ya kutokata tamaa. Kanisa na misikiti panarejelewa kama mahali patakatifu ambapo wanajamii wa jamii yetu hujifunzia maadili. Zaidi ya hayo kuna shule mbalimbali katika jamii yetu. Shule ni mahali muhimu katika jamii yetu kwa sababu zinasaidia kuelimisha wanajamii yetu na kuwafunza stadi kadhaa za kimaisha kama vile, kutafakari, kuwasiliana vizuri na kuwa wabunifu.

Isitoshe, kuna mahali kama masoko, vituo vya polisi, vyoo vya umma na kadhalika ambavyo husaidia wanajamii yetu.

Hospitali ya Kitagata iko upande wa Magharibi wa nyumbani kwetu ilhali ile ya Kabwohe iko upande wa Mashariki. Ukitoka upande wa Mbarara kuelekea Kasese, hospitali ya Kabwohe itakuwa upande wako wa kulia ambayo ni sehemu ya Mashariki. Kutoka nyumbani kwetu

kwenda shuleni ninakosomea, unaelekea upande wa kaskazini mpaka unapofika kituo cha polisi. Unapofika hapo, unapinda kushoto na kuenda upande wa Magharibi ya Kaskazini. Binamu yangu yeye anasomea katika shule ya Kibingo ambayo iko upande wa Kusini ya Magharibi kutoka kwetu. Kutoka kwetu kufika shuleni kwake, unatumia dakika ishirini pekee ukiwa unatembea kwa miguu.

1. Washirikishe kutafuta maneno mapya kutokana na makala na pia welekeze kutafuta maana ya maneno hayo kwa kutumia kamusi.
2. Waelekeze kuelezea ujumbe watakaopata baada ya kusoma makala hiyo.
3. Waongoze kuelezea jinsi wanavyoweza kuelekeza mtu kufika kwao.

**Sarufi:**

**Funzo g: Kutambua na kutumia vitenzi mbalimbali katika sentensi**

**Shughuli 7.2 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, waongoze kusoma na kujadili matumizi ya vitenzi vya aina zifuatazo**;**

**i. Vitenzi Halisi**

Hivi ni vitenzi vinavyorejelea kitendo moja kwa moja. Vitenzi halisi vinapoambatanishwa na vitenzi vidogo katika sentensi, huitwa vitenzi vikuu.

k.m: *soma, kula, sikiza*

- Mchezaji wa riadha alirejea jana kutoka ng'ambo.
- Mama atapikia wageni.
- Fungua mlango wa jikoni.

**ii. Vitenzi Visaidizi**

Vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi halisi (vitenzi vikuu) katika sentensi ili kuleta maana inayokusudiwa kulingana na wakati au hali.

k.m: *-kuwa, -ngali,*

- Jua lilikuwa limewaka sana mchana wote.
- Tajiri wake angali anamsumbua na mshahara.

**Taz:** Kitenzi ni neno linalosimamia kitendo. Kila kitenzi huwa na shina la kitenzi (sehemu ndogo zaidi ya kitenzi ambayo ndiyo huwakilisha tendo hilo). Shina la kitenzi huambatanishwa na viambishi ili kutoa maana iliyokusudiwa kama vile mtendaji, mtendewa, wakati kitendo kinafanyika na pia kauli ya kitenzi hicho.

1. Waongoze wanafunzi kutunga sentensi angalau tano kwa kutumia vitenzi mlivyojadili hapo juu.

2. Waelekeze wanafunzi kushirikiana kutunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.

(a) andika
(b) -kuwa
(c) endesha
(d) -ngali
(e) Pika

3. Hakikisha sentensi walizotunga ni sahihi

**Funzo h:**
**i. Kutumia vipatanishi vya nomino vya ngeli ya u-i katika sentensi**
**Shughuli 8.2 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, waongoze wanafunzi kusoma na kujadili maana ya nomino zifuatazo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mkeka | mikeka |
| mlima | milima |
| mti | miti |
| mkono | mikono |
| mkono | mikono |
| mkebe | mikebe |
| mkoba | mikoba |
| mkuki | mikuki |

2. Waongoze wanafunzi, kutafuta nomino za ngeli ya u-i na mziandike katika umoja na wingi.

3. Washirikishe wanafunzi katika kikundi kusoma na kutambua matumizi ya nomino za ngeli ya **u-i** katika sentensi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufuatao.

| umoja | | | wingi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **nomino** | **vimilikishi** | **viwakilishi** | **nomino** | **vimilikishi** | **viwakilishi** |
| Mgongo | | unauma | Migongo | | inauma |
| Mwembe | wangu | utavunjika | Miembe | yetu | itavunjika |
| Mpira | | ulipasuka | Mipira | | ilipasuka |
| Mkufu | wako | unatingika | Mkufu | yenu | inatingika |
| Mkebe | | unapiga kelele | Mikebe | | inapiga kelele |
| Mkoba | wake | una rangi nzuri | Mikoba | yao | ina rangi nzuri |
| Mkuki | | una ukali sana | Mikuki | | ina ukali sana |

| umoja | | | | wingi | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **nomino** | **vionyeshi** | | **vivumishi** | **nomino** | **vionyeshi** | | **vivumishi** |
| Mshipi | | | mrefu | Mishipi | | | mirefu |
| Mkeka | huu | | mzuri | Mikeka | hii | | mizuri |
| Mlima | | | mdogo | Milima | | | midogo |
| Mti | huo | **ni** | mzito | Miti | hiyo | **ni** | mizito |
| Mchoro | | | mkubwa | Michoro | | | mikubwa |
| Mlango | ule | | mdogo | Milango | ile | | midogo |
| Mwezi | | | mfupi | Miezi | | | mifupi |

4. Waongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi angalau kumi kutokana na majedwali mliyosoma hapo juu.
5. Hakikisha sentensi wanazotunga ni sahihi. Wakosoe walio na changamoto katika utungaji wa sentensi.

**ii.Uakifishaji**

**Shughuli 9.2 Kusoma na Kuandika**

Washirikishe wanafunzi katika makundi yao, kutunga sentensi angalau mbili kwa kila alama ya uakifishaji zifuatazo.

| |
|---|
| nukta (.) , nuktapacha (:), mkato (,) , mshangao (!) , kiulizi (?) , mabano ( ) , alama ya nukuu (" "), nuktamkato (;), |

Kwa mfano,

**Nukta** (.)

Kituo cha **nukta** kitatumika kama ifuatavyo:

(i) Mwishoni mwa neno, tungo au kifungu chenye kuleta maana kamili.
Mfano: Tulipofika, tulimwona.
(ii) Wakati wa kuandika herufi za vifupisho.
Mifano: N.B., A.D., B.Sc., Ph.D., k.v., k.m.
(iii) Wakati wa kuandika ili kutenga kiasi cha fedha, vipimo mbalimbali vya desimali, na pia kutenga saa na dakika. Mifano: shillingi 82.55, saa 12.15, kilogramu 2.73.

**Nuktapacha (:)** Kituo cha **nuktapacha** kitatumika kama ifuatavyo:

(i) Baada ya neno au kifungu cha maneno kinachofuatwa na maelezo au ufafanuzi zaidi.
Mifano: Alipofika sokoni alijipatia mahitaji yafuatayo: nyanya, vitunguu, nyama na matunda; Ili kufika huko, fuata njia ifuatayo: pita kushoto, vuka mto, na pinda kulia.
(ii) Baada ya kuandika jina la mhusika katika tamthiliya.
Mfano: JUMA: Unatoka wapi?; MUKI: Popote tu!
(iii) Wakati wa kutenganisha tarakimu katika mazingira yafuatayo:

a) Kutenganisha sura na aya, hasa katika Maandiko Matakatifu.
Mifano: AL - MAIDA: 96 - 100; LUK. 7: 10-18
b) Kutenganisha dakika na sekunde. Mfano: Saa 2.24:05

**Mkato (,)** Kituo cha **mkato** kitatumika kama ifuatavyo:

(i) Kutenga vifungu vya maneno au sentensi tegemezi kutoka kifungu kikuu, ili maana ya sentensi nzima ieleweke vema na kwa urahisi zaidi.
(ii) Wakati wa kuorodhesha mambo, hasa kama yako katika mfululizo wa sentensi na hivyo hayakupangwa hima. Mfano: Huko sokoni nilinunua: samaki, ndizi, matunda, na mboga.

**Mshangao (!)** Kituo cha **mshangao** kitatumika kama ifuatavyo:

(i) Baada ya neno au usemi wa kushangaa, kushtuka au wenye hisi.

Mifano:

- Kumbe alikuwa mwizi wa siku nyingi!
- Lo! Maskini mjomba wangu!

**Kiulizi (?)** Ni sawa na **Kiulizo,** au **alama ya kuuliz ambacho** kitatumika kama ifuatavyo:

(i) Kuonyesha neno au sentensi iliyokusudiwa kuwa swali.

Mifano:

- Sawa? Kweli? Ndivyo?
- Je, tuondoke lini?

Ili kuzingatia matumizi sahihi, **kiulizi** kiwekwe mwishoni mwa sentensi na si baada ya neno *Je*. Mkato unaweza kuwekwa baada ya *Je*. Pia *Je* yaweza ikawekwa mwishoni mwa neno au usemi unaokusudiwa kuwa swali.

**Mabano ( )**

Kituo cha **mabano** kitatumika kama ifuatavyo:

Kuhifadhi usemi, taarifa au maelezo ya nyongeza katika sentensi. Nyongeza yaweza kuwa bezo, mshangao au msisitizo wa mwandishi. Mifano:

- Nchi yetu (yaani Tanzania) ina utajiri mwingi wa maliasili.
- Yuleyule muuaji (ni ajabu na kweli!) alipandishwa cheo.

***Zingatia:*** Kwa kuwa Mabano huweza kuondolewa na maana ya sentensi ikabaki ileile, ni muhimu kuzingatia kwamba Mabano yatumike pale tu inapolazimu.

**Mnukuo (" ")** **Mnukuo,** au **Alama za usemi,** utatumika kama ifuatavyo:

(i) Zitatumika alama mbilimbili mwanzoni na mwishoni mwa usemi ulionukuliwa au kukaririwa.
Mfano: Mwalimu alisema, "Wanafunzi wazembe ni sumu kwa shule yetu."

**Deshi (—)** Kituo cha **deshi**, pia huitwa **kistari kirefu**, kitatumika kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Kama kitumikavyo kituo cha mabano, kituo cha deshi hutumika ili kuongeza taarifa au maelezo mengine yahusuyo usemi, neno au sentensi iliyotangulia. Kwa kawaida deshi mbili hutumika, yaani mwanzoni na mwishoni mwa maelezo ya nyongeza, iwapo maelezo hayo yapo katikati ya sentensi. Mifano:

- Nchi yetu — yaani Tanzania — ina utajiri mwingi wa mali asili.
- Alipoingia nyumbani akajitupa kitandani — kumbe mlango uko wazi.

**Kiungo (-)** Kituo hiki pia huitwa **kistari kifupi** au **kistariungio** hasa kukitofautisha na deshi ambayo pia hujulikana kama kistari kirefu.

**Kiungio** kitatumika kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Wakati wa kukata neno, hasa kwenye ukingo wa kulia wa karatasi, kutokana na kukosekana nafasi ya kuliandika zima.

(ii) Wakati wa kuonyesha kipindi, umbali, au muhula baina ya nyakati mbili. Katika mazingira haya kiungio hutumika badala ya maneno “hadi” au “mpaka”.

Mifano: Mwaka 1914 - 1918
Kurasa 5 - 17.

**Apostrofi (‘)** Kituo hiki kitatumika kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Kuonyesha matamshi ya king’ong’o.
Mifano: ng’ombe, ng’ambo, mgong’oto, ng’ang’ania, mkong’oto, n.k.

(ii) Kuonyesha nafasi ya herufi au tarakimu iliyoachwa. Mifano: ‘79 = 1979
N’sharudi = nimekwisharudi.

**Nuktakatishi (...)** Kwa kawaida kituo hiki hutumia nukta tatu au zaidi zenye kufuatana.

(i) Kituo hiki huonyesha dukuduku la usemi uliokatishwa na zitatumika kwa usemi uliokatishwa lakini unaojulikana kwa wengi; mathalan methali, nahau, kibwagizo, n.k.

Mfano: Mtoto wa nyoka .... (Methali).

(ii) Kuonyesha maelezo, mazungumzo, n.k. yaliyochanganyika na hali ya kuvuta maneno au kuvuta subira katika tabia ya msemaji. Mifano:

- Mu ... mu ... mukinipacha ... chakula nitasema (kigugumizi)
- Mara mwanzishaji akasikika: Tayari... moja ... mbili... tatu ...! (Mashindano ya mbio).

**Nuktamkato (;)** Kituo hiki kitatumika kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Kuunga mawazo mawili mbalimbali katika sentensi ambatano zilizotumika.
Mfano: Sisi si panya; wao si paka.

(ii) Kutenga vifungu vya sentensi ambatano moja ambayo ni ndefu mno na ambayo kwa kutumia kituo cha Mkato peke yake maana yake bado isingeeleweka kwa urahisi. Mfano: Hukuhakihakikisha kwamba haonekani, alikwenda pale mlangoni; akaufungua polepole.

**Kinyota (*)**

**Kinyota**, ambacho pia hujulikana kama **Asteriki**, ni kituo ambacho kitatumika kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Kuonyesha kuwa neno lililotiliwa alama hiyo limepewa maelezo zaidi. (Tazama "Uandikaji wa Fafanuzi"). Alama hii itawekwa baada ya herufi ya mwisho ya neno linalohusika, kwa juu.
Mfano: Kimwaga* huyu!

Washirikishe wanafunzi katika makundi yao kuakifisha sentensi hizi.

Hakikisha wametumia alama za uakifishaji kwa usahihi.

(i) mgeni aliendа sokoni na kununua viazi nyama nyanya na vitunguu
(ii) lo ni nani aliyekuumiza hivi alisema shangazi
(iii) yule mtoto anapenda kusoma kwa bidii
(iv) daktari richard anamtibu agnes
(v) anaaitwa wakabi anatoka jijini kampala

**Funzo i: Kuandika insha**

**Shughuli 10.2 Kuandika**

Katika vikundi vyao waongoze wanafunzi kujadiliana na kuandika insha kuhusu mahali muhimu katika jamii zao.

**Zingatia**

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. Woongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi.

Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

Waongoze na kuwashirikisha wanafunzi kusoma na kutambua kinachotakikana kutokana na shughuli jumlishi. Kisha kila mwanafunzi afanye shughuli jumlishi yake.

**Shughuli Jumlishi**

Mama yako ni mtumishi wa umma. Yeye ni mfanya kazi wa serikali. Amehamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine. Huko alikohamishwa, amehama na familia yake.

a) Unafikiri mnafaa kujua mahali gani muhimu katika mazingira mlikokwenda wewe na familia yako?
b) Kwa kurejelea mahali muhimu katika mazingira yako, eleza sababu mbalimbali kwa nini ni muhimu kutambua mahali muhimu katika mazingira yako.
c) Kwa kuzingatia alama za uakifishaji, andika insha ya maelezo ukimwelezea rafiki yako unayesoma naye jinsi anavyoweza kutoka shuleni na kukutembelea nyumbani kwenu.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu;*

a. Msamiati wa mahali muhimu.
b. Sehemu mbalimbali za dira.
c. Shughuli zinazofanyika katika mahali muhimu.
d. Sehemu muhimu mbalimbali kwa kutumia dira.
e. Usomaji wa makala na kujibu maswali.
f. Matumizi ya vitenzi mbalimbali katika sentensi.
g. Matumizi ya vipatanishi vya nomino katika sentensi za ngeli ya **u–i**.
h. Alama zote za uakifishaji katika sentensi na vifungu vya maneno.
i. Vipengele muhimu vya uandishi wa insha ya mwongozo.
j. Uandishi insha ya mwongozo.

Kuhusu Shughuli jumlishi iliyo juu, utatumia jedwali la kupimia umilisi wa mwanafunzi. Umilisi wa kila mwanafunzi utapimwa kulingana na kila kipengele cha tathmini kilichomo katika shughuli jumlishi. Kwa mfano, mwanafunzi ambaye atapata alama 2/3 au zaidi kutokana na (3) ambazo zinatarajiwa, huyo atachukuliwa kuwa amepata umilisi lengwa. Yule ambaye atapata alama ya chini, atastahili kuongozwa tena katika kufanya marudio na marekebisho kwa kurejelea vipengele vya mada ambavyo hajaelewa ili apate umilisi lengwa.

| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1**.** **Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| Kutaja mahali muhimu katika mazingira yao. | - Mwanafunzi atakayeweza kutaja mahali muhimu katika mazingira yake angalau 8, mpe 3/3.<br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja mahali muhimu katika mazingira angalalau 6, mpe 2/3.<br><br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja mahali muhimu katika mazingira yake angalau 3-4, mpe 1/3. | Mwanafunzi atakayeweza kutaja mahali muhimu muhimu katika maelezo na jinsi maelezo yake yanavyoambatana kiutaratibu.<br><br>-Aliye onyesha muumano wa mawazo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Aliye onyesha muumano wa mawazo kwa kiwango cha wastani mpe 2/3.<br><br>- Aliye onyesha muumano wa mawazo kwa kiwango cha chini, mpe 1/3. | Mwanafunzi ambaye ataweza kutaja umuhimu wa mahali muhimu kimaelezo au kimaandishi kwa kuzingatia sarufi sahihi, alama za uakifishaji, upatanisho wa ngeli ya u-i kwa usahihi.<br><br>-Atakaye timiza haya yote kwenye kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Atakaye timiza haya yote kwenye kiwango cha wastani mpe 2/3.<br><br>Atakaye timiza haya yote kwenye kiwango cha chini, mpe 1/3. | Mwanafunzi ambaye ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |
| Kwa kurejelea mahali muhimu | - Mwanafunzi ambaye | - Mwanafunzi ambaye ataweza | Mwanafunzi ambaye | Mwanafunzi ambaye |


| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1. **Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| katika mazingira yako, eleza sababu mbalimbali kwa nini ni muhimu kutambua mahali muhimu katika mazingira yako. | ataweza kuelezea umuhimu wa mahali muhimu kwa kurejelea ngalau mahali muhimu 8, mpe 3/3.<br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kuelezea umuhimu wa mahali muhimu kwa kurejelea ngalau mahali muhimu 5-6, mpe 2/3.<br><br>- Mwanafunzi ambaye ataweza kuelezea umuhimu wa mahali muhimu kwa kurejelea mahali muhimu ngalau 3-4, mpe 1/3 | kutaja na kueleza juu ya umuhimu wa mahali muhimu na jinsi maelezo yake yatakavyo umana kiutaratibu,<br><br>Aliyetimiza hayo kwenye kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha chini mpe 1/3 | ataweza kutaja maneno ya adabu au kuigiza vitendo sahihi vya maneno ya adabu, matumizi mazuri ya sarufi, alama za uakifishaji, upatanisho wa ngeli ya u-i kwa usahihi;<br><br>-Aliye tumia haya kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>- Aliye kwenye kiwango cha wastani mpe 2/3.<br>- Aliye kwenye kiwango cha chini, mpe 1/3. | ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |
| Kwa kuzingatia alama za uakifishaji, andika insha ya maelezo ukimwelezea rafiki yako unayesoma | - Mwanafunzi ambaye ataweza kuelezea kwa ufasaha na | - Mwanafunzi ambaye ataweza kuelezea kwa ufasaha na maelezo yake yameonyesha | - Mwanafunzi ambaye ataweza kuelezea kwa ufasaha na maelezo yake | Mwanafunzi ambaye ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo |

| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1**.** **Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| naye jinsi anavyoweza kutoka shuleni na kukutembelea | maelezo yake yanaeleweka<br><br>Aliyetimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha chini mpe 1/3 | muumano na mfuatano mzuri.<br><br>Aliyetimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha chini mpe 1/3 | yameonyesha upatanisho wa kisarufi wa u-i, matumizi ya alama za uakifishaji kwa namna inayostahili.<br><br>Aliyetimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Aliye kwenye kiwango cha chini mpe 1/3 | hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |

Baada ya kutambua kiwango cha umilisi wa mwanafunzi wako, utaunganisha na kujumlisha alama aliyopata kutokana na uwiano, muumano, uhakika pamoja na ile alama moja ya ubora zaidi ambayo atapata iwapo atakuwa amepitisha au kuongeza majibu ambayo hayakuwa katika matarajio yako. Baada ya kuzijumlisha, utaziandika juu ya alama tarajiwa zote kwa jumla na kisha uzidishe tatu. I wapo vipengele ni vingi, utafanya kama hapo juu na kisha utaunganisha alama za vipengele vya tathmini na mbalimbali ambavyo viko katika shughuli jumlishi na kisha jumla yake kuiandika kiwastani.

Alama ya mwisho utakayopata, ndiyo utahifadhi katika rekodi ya kumbukumbu ya tathmini ya wanafunzi.

# MADA KUU 1.3 HESABU



**Misamiati Msingi**

hasi
chanya
shufwa
witiri

Mada hii itakuwezesha:

a. Kuhesabu tarakimu kutoka 1-1000.
b. Kulinganisha tarakimu na vitu vilivyoandikwa nambari au tarakimu hizo.
c. Kutofautisha alama za hesabu mbalimbali.
d. Kutambua siku za wiki kupitia mfumo wa kiarabu.
e. Kueleza saa kwa kutumia mfumo wa kiswahili.
f. Kusoma makala yanayohusu hesabu na kujibu maswali.
g. Kutambua vivumishi vya idadi, sifa, na viulizi na kuvitumia katika sentensi.
h. Kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya li–ya katika sentensi.
i. Kuandika insha ya mwongozo ya ratiba yake ya kila siku.

**Utangulizi**

Katika mada hii, wanafunzi waongozwe kuhusu uzuri wa kujua kuhesabu. Watambue jinsi hesabu zinavyotumika katika kuhesabu pesa na na katika shughuli nyingine mbalimbali.

**Maandalizi pendekezwa ya mwalimu**
Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Kanda za sauti
- Kadi zenye maadishi ya sauti mbalimbali za Kiswahili
- Chati
- Michoro/picha
- Kanda za video
- Projekta
- Kamusi

**Funzo a: Kuhesabu tarakimu**

**Shughuli 1.3: Kusikiliza na kuzungumza**

Katika makundi yao, washirikishe wanafunzi kusoma na kuhesabu tarakimu zifuatazo.

| | |
|---|---|
| 0 | Sufuri |
| 1 | Moja |
| 2 | Mbili |
| 3 | Tatu |
| 4 | Nne |

| | |
|---|---|
| 5 | Tano |
| 6 | Sita |
| 7 | Saba |
| 8 | Nane |
| 9 | Tisa |

**Taz**; Kati ya nambari hizi kuna *nambari shufwa* na *nambari witiri.*

Nambari shufwa ni nambari ambazo huweza kugawiwa mbili bila kuacha baki kama vile; 2,4,6,8.

Nambari witiri ni nambari ambazo haziwezi kugawiwa mbili kama vile 1 au baada ya kuzigawa na mbili zinaacha baki la 1 kama vile; 3,5,7,9.

Nambari shufwa ni; 2,4,6,8 na kadhalika.

Nambari witiri ni; 1,3,5,7,9 na kadhalika.

Halafu kuna nambari hasi (-) mfano -1(hasi moja) na nambari chanya (+) mfano +2 (chanya mbili).

Waelekeze wanafunzi kusoma na kuhesabu tarakimu zifuatazo

| | |
|---|---|
| 10 | Kumi |
| 11 | Kumi na moja |
| 12 | Kumi na mbili |
| 13 | Kumi na tatu |
| 14 | Kumi na nne |
| 15 | Kum na tano |
| 16 | Kumi na sita |
| 17 | Kumi na saba |
| 18 | Kumi na nane |
| 19 | Kumi na tisa |

Washirikishe wanafunzi kujaza tarakimu katika mapengo

| | |
|---|---|
| 20 | Ishirini |
| 21 | Ishirini na moja |
| 22 | |
| 23 | |
| 24 | |
| 25 | |
| 26 | |
| 27 | |
| 28 | |
| 29 | Ishirini na tisa |

Washirikishe kujaza mapengo kwa kuandika maneno ya tarakimu katika majedwali yafuatayo.

**Nambari 30-39**

| | |
|---|---|
| 30 | Thelathini |
| 31 | Thelathini na moja |
| 32 | Thelathini na mbili |
| 33 | |
| 34 | |
| 35 | Thelathini na tano |
| 36 | Thelathini na sita |
| 37 | |
| 38 | |
| 39 | Thelathini na tisa |

**Nambari 40-49**

| | |
|---|---|
| 40 | Arubaini |
| 41 | Arubaini na moja |
| 42 | |
| 43 | |
| 44 | Arubaini na nne |
| 45 | Arubaini na tano |
| 46 | Arubaini na sita |
| 47 | |
| 48 | |
| 49 | Arubaini na tisa |

**Funzo b: Kulinganisha tarakimu na maneno**

**Shughili 2. 3 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, waongoze kuhesabu tarakimu zifuatazo. Hakikisha wanatamka vizuri.

**Nambari 50-59**

| | |
|---|---|
| 50 | Hamsini |
| 51 | |
| 52 | Hamsini na mbili |
| 53 | |
| 54 | |
| 55 | |
| 56 | |
| 57 | Hamsini na saba |
| 58 | |
| 59 | |

**Nambari 60-69**

| | |
|---|---|
| 60 | Sitini |
| 61 | Sitini na moja |
| 62 | |
| 63 | |
| 64 | |
| 65 | |
| 66 | |
| 67 | |
| 68 | Sitini na nane |
| 69 | Sitini na tisa |

**Nambari 70-79**

| | |
|---|---|
| 70 | Sabini |
| 71 | |
| 72 | |
| 73 | |
| 74 | |
| 75 | |
| 76 | Sabini na sita |
| 77 | Sabini na saba |
| 78 | |
| 79 | Sabini na tisa |

| | |
|---|---|
| 80 | Themanini |
| 81 | |
| 82 | |
| 83 | |
| 84 | |
| 85 | |
| 86 | |
| 87 | |
| 88 | |
| 89 | Themanini na tisa |

| | |
|---|---|
| 90 | Tisini |
| 91 | Tisini na moja |
| 92 | |
| 93 | |
| 94 | |
| 95 | |
| 96 | |
| 97 | |
| 98 | |
| 99 | Tisini na tisa |

**Nambari 100-900**

| | |
|---|---|
| 100 | Mia moja |
| 200 | Mia mbili |
| 300 | Mia tatu |
| 400 | Mia nne |
| 500 | Mia tano |
| 600 | Mia sita |
| 700 | Mia saba |
| 800 | Mia nane |
| 900 | Mia tisa |

**Funzo c: Kutofautisha alama za hesabu**

**Shughuli 3.3 Kusikiliza na kuzungumza**

Katika makundi yao, waongoze wanafunzi kutambua alama za hesabu zifuatazo.

- Alama ya kuondoa -
- Alama ya kujumlisha +
- Alama ya kuzidisha ×
- Alama ya kugawanya ÷
- Alama ya mlinganyo =

1. Waelekeze wanafunzi kutumia alama za hesabu mbalimbali kupata matokeo mbalimbali

**Funzo d: Kutambua siku za wiki**

**Shughuli 4.3 Kuoma**

1. Waongoze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu siku za wiki zifuatazo

Leo - siku hiyo iliopo.

Jana - Siku kabla ya leo.

Juzi- Siku kabla ya jana.

Kesho - Siku baada ya leo.

Kesho kutwa - Siku baada ya kesho.

Mtondo - Siku baada ya kesho kutwa

Mtondogoo - Siku baada ya mtondo

Siku ya Sabato kwa Wakristo ni Jumamosi au Jumapili.

Waislamu huenda msikitini siku ya Ijumaa.

2. Katika makundi, washirikishe wanafunzi kujibu maswali yafuatayo;
3. Hakikisha kwamba wanafunzi wanajibu maswali yafuatao kulingana na muktadha.

(a) Leo ni siku gani? ………………………….……………….

(b) Jana ilikuwa siku gani? ……………………………………..
(c) Kesho itakuwa siku gani? …………………………………..
(d) Juzi ilikuwa siku gani? ………………………………………
(e) Kesho kutwa itakuwa siku gani? ………………………………

**Funzo e: Kueleza shughuli za siku**

**Shughuli: 5.3 Kusikiliza na kuzungumza**

Katika vikundi, waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu shughuli mbalimbali wanazofanya nyumbani kabla ya kuja shuleni na baada ya kurudi nyumbani.

Washirikishe wanafunzi kujadiliana kuhusu shughuli mbalimbali wanazofanya nyumbani hasa wakati wa wikiendi.

**i.** Waelekeze kuwasilisha matokeo yao darasani

**Funzo f: Kutamka miezi ya mwaka**
**Shughuli 6.3 Kusoma na kuandika**

1. Washirikishe wanafunzi kusoma na kujadili miezi ya mwaka

i. Mwezi wa kwanza wa mwaka ni Januari.
ii. Mwezi wa pili wa mwaka ni Februari.
iii. Mwezi wa tatu wa mwaka ni Machi.
iv. Mwezi wa nne wa mwaka ni Aprili.
v. Mwezi wa tano wa mwaka ni Mei.
vi. Mwezi wa sita wa mwaka ni Juni.
vii. Mwezi wa saba wa mwaka ni Julai.
viii. Mwezi wa nane wa mwaka ni Agosti.
ix. Mwezi wa tisa wa mwaka ni Septemba.
x. Mwezi wa kumi wa mwaka ni Oktoba.
xi. Mwezi wa kumi na moja wa mwaka ni Novemba.
xii. Mwezi wa kumi na mbili wa mwaka ni Desemba.

Msamiati unaohusiana na miezi ya mwaka

- Mwezi huu
- Mwezi ujao/ mwezi kesho- Baada ya mwezi huu
- Mwezi uliopita/ mwezi jana- Kabla ya mwezi huu

- Mwanzoni mwa mwezi
- Katikati mwa mwezi
- Mwishoni mwa mwezi

4. Katika makundi yao, washirikishe wanafunzi kujibu maswali yafuatayo kulingana na muktadha. Kwa mfano wakati wa kusoma funzo hilo;

(a) Mwezi huu ni mwezi wa……………………………………
(b) Mwezi wa kwanza una siku………………………………..
(c) Mwezi wa mwisho wa mwaka ni…………………………..
(d) Mwezi wa Oktoba una siku ……………………………….
(e) Mwezi ujao utakwa mwezi wa…………………………….

**Funzo g. Kueleza Saa**

**Shughuli 7.3 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao waelekeze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu msamiati unaohusiana na saa ufuatao.

Saa ni chombo ambacho huonyesha wakati.

Siku nzima ina saa ishirini na nne.

Msamiati unaotumiwa kwenye saa

Dakika - Saa moja ina dakika sitini.

Sekunde - Dakika moja ina sekunde sitini.

Nusu - Dakika thelathini.

Robo - Dakika kumi na tano.

Kasorobo - Dakika kumi tano kuingia saa nyingine.

Kamili - Hakuna dakika ambayo imepita kwenye saa.

Alfajiri - kati ya saa tisa na saa kumi na moja asubuhi.

Adhuhuri - Saa sita.

Mchana - Ni kipindi kinachoanzia kuchomoza kwa jua hadi kutua kwake/ Kipindi kilicho kati ya  Saa sita hadi saa tisa.

Jioni - Ni wakati baina ya alasiri na magharibi.


Usiku - Saa moja hadi saa tano.

Usiku wa manane - Saa saba hadi saa tisa usiku.

1. Katika makundi yao, waelekeze kushirikiana katika kutambua na kutaja saa mbalimbali zifuatazo;



Sasa ni saa ngapi?

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
|  |  | |

2. Katika makundi waelekeze kusoma, kuchora na kutaja saa zifuatazo

(a) Saa kumi na mbili kamili asubuhi.
(b) Saa kumi na moja na robo jioni.
(c) Saa nne na nusu usiku.
(d) Saa mbili na dakika ishirini asubuhi.
(e) Saa nane kasoro dakika kumi mchana.

**Funzo h: Kusoma kalenda**

**Shughuli 8.3: Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, waongoze wanafunzi kusoma, kutamka na kuandika tarehe zifuatazo kwa maneno

Jumamosi 10/3/1992 - Jumamosi tarehe kumi mwezi wa Machi mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na mbili.

Alhamisi 6/10/2000 - Alhamisi tarehe sita mwezi wa Oktoba mwaka elfu mbili.

Jumanne 25/4/2017 - Jumanne tarehe ishirini na tano mwezi wa Aprili mwaka wa elfu mbili kumi na saba.

1. Waongoze wanafunzi kusoma kutamka na kuandika tarehe zifuatazo katika tarakimu

i. Ijumaa tarehe thelathini mwezi wa Julai mwaka wa elfu moja mia nane themanini na nane.
ii. Jumatatu tarehe tatu mwezi wa Januari mwaka wa elfu mbili kumi na nane.
iii. Jumapili tarehe ishirini na nne mwezi wa Novemba mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na tisa.
iv. Jumatano tarehe kumi na saba mwaka wa Desemba mwaka wa elfu mbili na moja.
v. Alhamisi tarehe tisa mwezi wa Mei mwaka wa elfu moja mia sita sabini na nne.

2. Katika kikundi yao, washirikishe kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa katika makala hii.

**SIKU ZA WIKI**

Wiki/Juma ni muda wa siku saba. Katika lugha ya Kiswahili, wiki ina siku saba kwa ujumla. Siku ya kwanza katika kalenda ya Kiswahili ni Jumamosi. Jumamosi ni siku ambayo Wakristo wa dhehebu la Kiadventi huenda kanisani kuomba Mungu.

Siku ya pili katika lugha ya Kiswahili huitwa Jumapili. Hii ni siku ambayo Wakristo wengine kama vile Wakatoliki na Waprotestanti huenda kanisani kwa ajili ya kumwomba Mwenyezi Mungu na kumshukuru kwa mema ambayo amewajalia.

Siku ya tatu huitwa Jumatatu. Hii ni siku ya kufanya kazi. Wafanyakazi wote huenda kazini na wanafunzi huenda shuleni kusoma.

Siku ya nne katika lugha ya Kiswahili inaitwa Jumanne. Siku hii pia ni ya kufanya kazi. Vile vile, wanafunzi huenda shuleni kuhudhuria vipindi.

Siku ya tano katika lugha ya Kiswahili ni Jumatano. Hii ni siku ya kufanya kazi pia.

Siku ya Alhamisi ni siku ya sita katika wiki. Katika siku hii pia watu huenda kufanya kazi.

Siku ya Ijumaa ni siku ya saba ambayo ni ya mwisho katika wiki. Siku hii Waislamu huenda msikitini kuswali/ kufanya ibada ya swala ambayo ni ya lazima kwa kila mwislamu.

3. Katika kikundi chao, waelekeze kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa katika makala hii.

**i.** Wiki ina siku ngapi?
**ii.** Taja siku ya kwanza ya wiki katika lugha ya Kiswahili.
**iii.** Waadventi huenda kanisani siku gani?
**iv.** Je, Wakristo huenda kanisani kufanya nini? Taja hoja mbili.

**Sarufi**
**Funzo i; Kutambua vivumishi vya idadi na sifa**

**Shughuli 9.3 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, waongoze kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya vivumishi vya Idadi

Hutueleza zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi.

***a) Idadi Kamili***

Hii hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino. Kwa mfano: *tatu, mbili, kumi*

- Msichana mmoja amewauwa nyoka wawili
- Siku kumi zimepita tangu Bi Safina alipojifungua watoto watatu

***b) Idadi Isiyodhihirika***

Kivumishi hiki cha idadi huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili. Kwa mfano: *chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani*.

- Watu wachache waliohudhuria mazishi ya Kajuta walikula chakula kingi sana.
- Baba yao alikuwa mateka kwa miaka kadhaa.

1. Washirikishe kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya vivumishi vya sifa

Hivi ni vivumishi ambavyo hutoa sifa ya kitu, mtu, mahali, na kadahalika kwa mfano: *kizuri, kali, safi, mrembo*. Ni neno/maneno ambayo hutaja maana ya sifa ya nomino au kiwakilishi cha nomino jinsi kilivyo.

Mifano:

- Paka mwizi amelala jikoni
- Ugonjwa hatari umeukumba dunia
- Gari zuri limegongwa
- Nyumba kubwa imejengwa bondeni
- Kijana mpole kasusa kula

2. Waelekeze kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya viulizi vifuatavyo;

Viulizi ni maneno yanayotumika katika kuulizia kwa mfano: je, gani, lipi, nani, nini, wapi nk

**Mifano katika sentensi;**

**1. Je?**

i) Je, ulimwona mwalimu wa Kiswahili?

ii) Mlifanyaje mtihani?

2. **Nani?**

i) Nani anafundisha Kiswahili?

ii) Nani ananiita?

iii) Unaitwa nani?

3. **Nini?**
    i) Umenunua nini?
    ii) Tutakula nini?
    iii) Unataka nini?
4. **Lini?**
    i) Utarudi lini?
    ii) Mwalimu atafika lini?
    iii) Mtanitembelea lini?
5. **Gani?**
    i) Huyu ni mtu gani?
    ii) Unakula chakula gani?
    iii) Nikupe kitu gani?
6. **Namna gani?**
    i) Tutapita namna gani?
    ii) Unakula namna gani?
    iii) Umeketi namna gani?
7. **Kwa nini?**
    i) Kwa nini ulitoroka?
    ii) Kwa nini mnapiga kelele?
    ii) Kwa nini ulikataa kunisaidia?
8. **Tangu lini?**
    i) Tangu lini umekuwa hapa?
    ii) Wamelala tangu lini?
    iii) Amekuwa mgonjwa tangu lini?
9. **Mara ngapi?**
    i) Unakula mara ngapi?
    ii) Mwanafunzi yule alitoroka mara ngapi?
    iii) Mariam amelia mara ngapi?
10. **-ngapi?**
    i) Mmesoma vitabu vingapi?
    ii) Unacheza michezo mingapi?
    iii) Mna walimu wangapi shuleni?
11. **-pi?**
    i) Unataka mwalimu yupi?
    ii) Ameandika vitabu vipi?
    iii) Wamenunua gari lipi?

3. Washirikishe wanafunzi katika makundi yao kutunga angalau sentensi tatu kwa kila kiulizi walichosoma.

**Funzo j: Kutunnga sentensi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi.**

**Shughuli 10.3 Kusoma na kuandika**

Katika makundi yao, washirikishe wanafunzi kujadiliana na kusoma kuhusu matumizi ya vipatanishi vya kisarufi vya li-ya.

Ngeli hii hujumuisha nomino za baadhi ya vitu visivyo hai pamoja na nomino za ukubwa za ngeli mbalimbali. Kuna baadhi ya nomino za ngeli hii ambazo huanza kwa kiambishi **Ji** katika umoja na nyingine nyingi hazina kiambishi hiki. Hata hivyo, wingi wa nomino zote katika ngeli hii, huchukua kiambishi awali **Ma** au **Me** katika wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| jicho | macho |
| jiwe | mawe |
| jino | meno |
| jibu | majibu |
| jipu | majipu |
| jiko | meko |
| jina | majina |
| jicho | macho nk |
| yai | mayai |
| bega | mabega |
| chungwa | machungwa |
| daftari | madftari |
| jambo | mambo |
| shavu | mashavu |
| gurudumu | magurudumu |

1. Washirikishe wanafunzi kutafuta majina mengine ya li-ya kutokana na kamusi

3. Waelekeze wanafunzi kusoma na kujadili sentensi zifuatazo kutokana na majedwali kisha washirikishe kuunganisha vipengele mbalimbali ili kutunga sentensi zenye maana. Hakikisha wanatunga sentensi sahihi.

| **Umoja** | | | **wingi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **nomino** | **vimilikishi** | **viwakilishi** | **nomino** | **vimilikishi** | **viwakilishi** |
| Jina | | **li**nauma | Jina | | **ya**nauma |
| Jicho | langu | **li**napendeza | Jicho | yetu | **Ya**napendezwa. |
| Yai | | **li**likatwa | Yai | | **ya**likatwa |
| Bega | lako | **li**nametameta | Bega | yenu | **ya**nametameta |
| Chungwa | | **li**meisha | Chungwa | | **ya**meisha |
| Daftari | lake | **li**najibiwa | Daftari | yao | **ya**najibiwa |
| Gunia | | **li**menunuliwa | **Ma**gunia | | **ya**menunuliwa |

| **Umoja** | | | | **wingi** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **nomino** | **vionyeshi** | | **vivumishi** | **nomino** | **vionyeshi** | | **vivumishi** |
| Jina | | | kubwa | Jina | | | makubwa |
| Jicho | hili | | zito | Jicho | haya | | mazito |
| Yai | | | dogo | Yai | | | madogo |
| Bega | hilo | ni | refu | Bega | hayo | ni | marefu |
| Chungwa | | | kubwa | Chungwa | | | makubwa |
| Daftari | lile | | gumu | Daftari | yale | | magumu |

2. Waongoze wanafunzi kutunga sentensi angalau kumi kutokana na kila jedwali mlilosoma hapo juu. Hakikisha kwamba sentensi ni sahihi.

**Funzo k: Kuandika Insha**

**Shughuli 11.3 Kuandika**

Katika makundi yao, washirikishe wanafunzi kujadiliana na kuandika insha ya mwongozo kuhusu ratiba yao ya kila siku kuanzia wakati wanapoamka asubuhi hadi wakati wanapoelekea kulala usiku.

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. Woongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi.

Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli Jumlishi**

Siku ya likizo kuisha ni kesho. Leo umeomba pesa kwa mzazi wako ili uende sokoni kununua baadhi ya vitu utakavyotaka kutumia shuleni.

d) Elezea na kisha undike insha ukionyesha siku yenyewe pamoja na tarehe utakaporudi shuleni. Ungependa utoke nyumbani saa ngapi na mwendo unaweza kukuchukua saa ngapi kufika shuleni? Katika insha yako, zingatia matumizi ya vivumishi vya idadi, sifa na viulizi.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu;*

a. Kuhesabu tarakimu kutoka 1-1000.
b. Kulinganisha tarakimu na vitu vilivyoandikwa nambari au tarakimu hizo.
c. Kutofautisha alama za hesabu mbalimbali.
d. Kutambua siku za wiki kupitia mfumo wa kiarabu.
e. Kueleza saa kwa kutumia mfumo wa kiswahili.
f. Kusoma makala yanayohusu hesabu na kujibu maswali.
g. Kutambua vivumishi vya idadi, sifa, na viulizi na kuvitumia katika sentensi.
h. Kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya li–ya katika sentensi.
i. Kuandika insha ya mwongozo ya ratiba yake ya kila siku

Kuhusu Shughuli jumlishi iliyo juu, utatumia jedwali la kupimia umilisi wa mwanafunzi. Umilisi wa kila mwanafunzi utapimwa kulingana na kila kipengele cha tathmini kilichomo katika shughuli jumlishi. Kwa mfano, mwanafunzi ambaye atapata alama 2/3 au zaidi kutokana na (3) ambazo zinatarajiwa, huyo atachukuliwa kuwa amepata umilisi lengwa. Yule ambaye atapata alama ya chini, atastahili kuongozwa tena katika kufanya marudio na marekebisho kwa kurejelea vipengele vya mada ambavyo hajaelewa ili apate umilisi lengwa.


| **Matarajio** | Mbinu ya utuzaji 1**. Uwiano** | Mbinu ya utuzaji 2. **Muumano** | Mbinu ya utuzaji 3. **Uhakika** | Mbinu ya utuzaji 4. **Ubora zaidi** |
|---|---|---|---|---|
| Elezea na kisha undike insha ukionyesha siku unaporudi shuleni yenyewe pamoja na tarehe utakaporudi shuleni. Ungependa utoke nyumbani saa ngapi na mwendo unaweza kukuchukua saa ngapi kufika shuleni? Katika insha yako, zingatia matumizi ya vivumishi vya idadi, sifa na viulizi. | - Mwanafunzi atakayeweza kuandika insha kwa kudhihirisha tarehe zinazohitajika, saa zinazohitajika na maagizo mengine.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha chini mpe 1/ | Mwanafunzi atakayeweza kuandika insha kwa kudhihirisha muumano na mtiririko wa mawazo kwa kuzingatia maagizo kutokana na swali.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha chini mpe 1/ | Mwanafunzi atakayeweza kuandika insha kwa lugha sahihi, matumizi bora ya upatanisho wa kisarufi, uakifishaji, matumizi bora ya vivumishi, viulizi na vipengele vingine vya lugha.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha juu, mpe 3/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha kati, mpe 2/3.<br><br>Atakayeandika insha yake kwa kutimiza hayo kwa kiwango cha chini mpe 1/ | Mwanafunzi ambaye ataweza kuongezea maarifa zaidi ambayo hayakuwa katika matarajio yako, mpe alama 1 |

Baada ya kutambua kiwango cha umilisi wa mwanafunzi wako, utaunganisha na kujumlisha alama aliyopata kutokana na uwiano, muumano, uhakika pamoja na ile alama moja ya ubora zaidi ambayo atapata iwapo atakuwa amepitisha au kuongeza majibu ambayo hayakuwa katika matarajio yako. Baada ya kuzijumlisha, utaziandika juu ya alama tarajiwa zote kwa jumla na kisha uzidishe tatu. I wapo vipengele ni vingi, utafanya kama hapo juu na kisha utaunganisha alama za vipengele vya tathmini na mbalimbali ambavyo viko katika shughuli jumlishi na kisha jumla yake kuiandika kiwastani.

Alama ya mwisho utakayopata, ndiyo utahifadhi katika rekodi ya kumbukumbu ya tathmini ya wanafunzi.

# MUHULA WA PILI

# MADA KUU 1.4 WANYAMA NA NDEGE



**Misamiati Msingi**

Vikembe
Malighafi
Mahiri
Mazingira
Kitega
Uchumi

**Mada hii itakuwezesha;**

a. kutambua majina ya wanyama na ndege wa nyumbani na porini.
b. kueleza faida za wanyama na ndege.
c. kutambua vikembe mbalimbali.
d. kusoma na kujadili makala yanayohusu sifa za wanyama na ndege.
e. kubaini matumizi ya vivumishi vimilikishi katika sentensi.
f. kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya A–WA katika sentensi.
g. kuandika insha ya mwongozo kwa kufasiri michoro kuhusu wanyama na faida zao.

**Utangulizi**

Katika mada hii, mwanafunzi aweze kutambua na kubainisha wanyama wa nyumbani na wa porini pamoja na watoto wao. Mada hii vilevile iwawezeshe wanafunzi kutambua ndege wa nyumbani na wa porini pamoja na watoto wao. Pia mada hii iwawezeshe wanafunzi kutambua umuhimu wa wanyama na ndege kwa jamii.

**Maandalizi Pendekezwa ya mwalimu**

Katika mada hii, unaweza kuandaa na kutumia vifaa vifuatavyo:

- Michoro ya wanyama na ndege
- Chati
- Mazingira
- Vitu halisi
- Kanda za video
- Projekta

**Funzo a: Kutambua majina na ndege wa nyumbani**

**Shughuli 1.4: Kusikiliza na kuzungumza**

1. Katika funzo hili, wanafunzi watajifunza kuhusu wanyama na ndege wa nyumbani na wa porini. Ili kuwawezesha kuelewa vizuri,

(a) Waongoze katika vikundi vyao kujadili kuhusu wanyama wa nyumbani na kisha kila kikundi kitaje majina ya wanyama waliojadiliana. Baadhi ya majina ya wanyama wa nyumbani ni; ng'ombe, mbuzi, ngamia, kondoo, nguruwe, paka, sungura, mbwa, punda.


(b) Washirikishe katika mjadala kuhusu ndege wa nyumbani na kisha kila kikundi kitaje ndege waliojadiliana. Mifano ya ndege watakayotaja ni kama; kuku, jogoo, kifaranga, bata, njiwa, batamzinga, tausi.


(c) Tazameni michoro ya wanyama iliyopo hapa chini na kila mmoja ataje majina ya wanyama hao. Chagua jina sahihi kutoka yale uliyopewa katika boksi hapo chini.


a


b


c


d


e


f


g


h


i


g

| Nguruwe, Mbwa, Sungura, Ngamia, Kondoo, Paka, Punda, Farasi, Ng'ombe, Mbuzi |
|---|

Majibu kutoka kwa wanafunzi yanastahili kuwa:


| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Mbuzi | 2. Ng'ombe | 3. Punda | 4. Farasi |
| 5. Kondoo | 6. Paka | 7. Mbwa | 8. Sungura |
| 9. Nguruwe | 10. Ngamia | | |

2. Wanafunzi wakiwa katika jozi,
   (a) Hakikisha kuwa wanatoa milio ya wanyama au ndege na kila mmoja wao atoe milio ya wanyama wawili.
   (b) Waongoze katika kuigiza milio ya ndege wafuatao:1, 2, 5, 6. Kwa mfano;

| **Ndege** | **Mlio wake** |
|---|---|
| 1. **Kuku** | Kokokokoook |
| 3 **Jogoo** | Kokoriiikooo |
| 5 **Bata** | Gha gha gha/ kwak-kwak |
| 6 **Kifaranga** | Syoi--syoi |


   (c) Waongoze katika vikundi vyao kueleza umuhimu wa ndege 1, 4, na 7 kwa jamii. Kwa mfano,

| | |
|---|---|
| Ndege 1 | hutupa mayai, nyama na pesa |
| Ndege 4 | hutupa nyama, mayai na pesa |
| Ndege 7 | hutupa nyama, mayai, mbolea na pesa |



**a**


**b**


**c**



**d**



e



f



**g**

**Funzo b: Kutaja majina ya wanyama na ndege wa pori**

**Shughuli 2.4: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

Katika funzo hili, wanafunzi wanatakikana kutaja majina ya wanyama na ndege wa pori. Kwa hiyo, unafaa:


1. Kuwaongoza kujadiliana juu ya wanyama wa porini na kisha mmoja wao asimame mbele ya darasa na kutaja majina ya wanyama waliojadiliana. Kwa mfano, Simba, Ndovu, Mbogo, Chui, Pundamilia, Fisi, Kobe, Twiga, Mbwamwitu
2. Kuwaongoza wanafunzi katika vikundi vyao na uhakikishe kila kikundi kinachora majina ya baadhi ya wanyama na ndege wa porini na kuandika majina ya kila mmnyama na ndege waliochora.
3. Kuwashirikisha katika kujadili kuhusu michoro ya ndege na wanyama pori mliopewa hapa chini na kila kikundi kiandike majina ya wanyama na ndege hao. Mifano ni kama;




korongo



mwewe



simba



ndovu



bundi



tai



nyati



twiga



chui




chui- milia



punda-milia



ngiri


nyani


tumbiri


sokwe


fisi

**Funzo c: Kueleza faida za wanyama na ndege**

**Shughuli 3.4: Kusikiliza, kuzungumza na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi katika vikundi vyao,

(a) Kujadiliana kwa kina kuhusu faida za wanyama na ndege na kisha kila kikundi kiandike faida zake kwenye chati na kuzitundika ukutani. Kila kikundi kitembelee kazi za wengine zilizotundikwa ukutani na kulinganisha na zake. Mifano ya faida zinazotarajiwa ni kama;

- Baadhi ya wanyama hutupa nyama.
- Baadhi ya wanyama hutupa maziwa
- Wanyama hasa wa porini huvutia watalii ambao hutuletea pesa
- Wanyama hasa wa nyumbani hutupa mbolea
- Wanyama wa nyumbani hutupa pesa tukiwauza au tukiuza maziwa
- Ndege hutupa mayai, pesa, nyama, mbolea

(b) Kuangalia kwa makini na kujadiliana kuhusu jedwali na kisha kujibu maswali.

| | Mnyama | Faida |
|---|---|---|
| a) | Mbuzi | Nyama, maziwa , ngozi, mbolea. |
| b) | Ng'ombe | Maziwa, nyama, mbolea, ngozi. |
| c) | Punda | Kubeba mizigo, usafiri, mbolea. |
| d) | Farasi | Kubeba mizigo, usafiri, mbolea, michezo mbalimbali. |
| e) | Kondoo | Nyama, maziwa, sufu, ngozi, mbolea. |

| | | |
|---|---|---|
| f) | Paka | kushika panya. |
| g) | Mbwa | ulinzi na usalama. |
| h) | Sungura | nyama, mbolea. |
| i) | Nguruwe | nyama, mbolea. |
| j) | Ngamia | kubeba mizigo, usafiri, nyama, mbolea, ngozi. |

i. Waongoze kujibu “Ni wanyama gani walio na faida nyingi sana? Kwa nini unasema hivyo?” Mifano ya majibu ni kama:

- Ngombe kwa sababu hutupa maziwa, nyama, pesa, mbolea, hulipa mahari, n.k
- Farasi kwa sababu hubeba mizigo, hubeba watu, huliwa, hutupa mbolea, n.k

**ii.** Waongoze kuongeza kwa faida zilizotolewa kwa kila mnyama katika jedwali

**Funzo d: Kutambua vikembe mbalimbali**

**Shughuli 4.4: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

(a) Wakiwa katika jozi, waongoze wanafunzi kutumia kamusi, maktaba au mtandao kutafiti kuhusu vikembe mbalimbali. Baada ya utafiti, waongoze kuwasilisha majina ya vikembe darasani mbele ya wanafunzi wengine.

(b) Wakiwa katika vikundi, washirikishe katika kujadiliana na kuandika majina ya vikembe na kwa kila kikembe, waandike jina la mzazi wake.

**Funzo e: Kusoma Makala kuhusu sifa za wanyama na ndege**

**Shughuli 5.4: Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi, wakiwa katika vikundi vyao,kusoma taarifa ifuatayo na kisha wajibu maswali yanayofuata.

**Faida za wanyama wa nyumbani**

Wanyama wa nyumbani ni wale ambao wanakubali kufugika na kuridhiana na mwanadamu katika mazingira ya kinyumbani, bila ya madhara mabaya.

Wanyama hawa wafugwao wana faida chungu nzima kwa mwanadamu; kuna ngamia, ng’ombe, mbuzi, mbwa paka, sungura na wengineo. Miongoni mwao wamo waliwao na wale wasioliwa, ingawaje wasioliwa pia wana umuhimu wao mwingi kwa mwanadamu; kama vile mbwa ni mlinzi madhubuti, farasi naye ni hodari kwa ubebaji wa mizigo na usafiri. Paka ni msasi wa panya pamoja na faida nyingine nyingi.

Ama wale waliwao tukianza na ng’ombe ana manufaa makubwa katika harakati za ulimaji. Pakosekanapo trakta basi yeye huingia kazi, huchangia sehemu kubwa ya uchumi na maendeleo katika kilimo na ufugaji. Na kama ilivyo kawaida kuwa nyama zao ni kitowe, huliwa na kuuzwa pamoja na kutupa maziwa. Ngozi kama za ngamia, ng’ombe na mbuzi huleta pesa nyingi, kwani ni mali ghafi ya vifaa vingi kama vile viatu, mabegi, mikanda, majaketi, kofia, foronya za viti na kadhalika.

Ufugaji wa wanyama wote wa nyumbani waliwao na wasioliwa ni kitega uchumi kikubwa ambacho huleta maendeleo ya kiuchumi kwa mfugaji binafsi na taifa kwa ujumla.

**Waongoze wanafunzi kujibu maswali kutoka makala waliyosoma. Maswali ya kujibiwa ni yafuatayo:**

(a) Unaelewa nini kuhusu wanyama wa nyumbani kulingana na taarifa hii?

Mifano ya majibu:

- Wanyama wa nyumbani huishi nyumbani karibu na watu.
- Wanyama wa nyumbani ni wa muhimu kwa jamii kwa sababu ya faida walio nao kwa watu.
- Wanyama huvutia watalii ambao huleta pesa.

(b) Taja wanyama watano wa nyumbani waliwao.

Mifano ya majibu:

- Ng’ombe
- Mbuzi
- Kondoo
- Sungura

(c) Taja wanyama watatu wa nyumbani wasioliwa.

Mifano ya majibu:

- Mbwa
- Paka
- Panya wadogo

(d) Eleza faida tatu za ng’ombe.

Mifano ya majibu:

- Hutupa maziwa
- Hutupa nyama
- Hutupa pesa

(e) Ni vitu gani ambavyo hutengenezwa kwa ngozi za wanyama?

Mifano ya majibu:

Viatu

Mikoba

Nguo

Ngoma

**Sarufi:**

**Funzo f: Kutumia vivumishi vimilikishi katika sentensi**

**Shughuli 6.4: Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi katika makundi;

i. Kujadiliana na kutambua maana ya vivumishi vimilikishi huku mkitoa mifano.

- Vivumishi vimilikishi ni aina ya vivumishi vinavyoonyesha mmilikaji wa kitu au mtu. Huonyesha mwenyewe wa kitu au mtu. Mifano ni kama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| -angu | -etu |
| -ako | -enu |
| Ake | -ao |

ii. Kutumia vivumishi vimilikishi walivyotambua katika i. hapo juu kutunga sentensi wakitumia nomino za **a-wa** zinazotaja wanyama na ndege. Mifano ya sentensi ni kama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ng'ombe **wangu a**mezaa ndama wawili. | Ng'ombe **wetu wa**mezaa ndama wawili. |
| Simba **wako a**mekimbiza mtalii. | Simba **wenu wa**mekimbiza watalii. |
| Kuku **wake a**metaga yai. | Kuku **wao wa**metaga mayai |

**Funzo g: Kutumia vipatanishi vya nomino za ngeli ya a-wa katika sentensi**

**Shughuli 7.4: Kusoma na Kuandika**

Wanafunzi wakiwa katika vikundi,

i. Waongoze kujadiliana kuhusu nomino za ngeli ya a-wa zinazotaja majina ya wanyama na ndege na kisha waziandike nomino hizo katika madaftari yao.

Kwa mfano:

Ng'ombe, Kondoo, Simba, Chui, Fisi, Sungura

Kuku, Bata, Njiwa, Tausi, Batamzinga

ii. Washirikishe katika kutunga sentensi sahihi kwa kutumia vipatanishi vya kisarufi vya ngeli ya a-wa. Sentensi hizi ziandikwe kwa chati kwa umoja na wingi na kutundikwa ukutani ili vikundi vingine vilinganishe na zao.

Mifano ya sentensi ni kama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mbuzi wangu huyu ni mnono. | Mbuzi wetu hawa ni wanono. |

| | |
|---|---|
| Chui yule amekula kondoo wanke. | Chui wale wamekula kondoo wao. |
| Jogoo wake huyo anawika vizuri. | Jogoo wao hao wanawika vizuri. |

**Funzo h: Kuandika insha kutokana na ufasiri wa michoro.**

**Shughuli 8.4: Kuandika**

Waongoze wanafunzi katika vikundi,

- Kutazama kwa makini michoro iliyopo na kutunga insha inayolingana na michoro hiyo. Pitia pitia vikundi ukiwaelekeza kuhusu vijenzi vya insha nzuri, kwa mfano,

- Kichwa kilichoandikwa kwa herufi kubwa
- Mwili wenye mtiririko mzuri wa mawazo; wazingatie tahajia, uakifishaji, sarufi.n. k
- Tamati inayotoa muhtasari wa insha
- Wazingatie idadi ya maneno waliyoagizwa kutumia.

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewe wanachoagizwa kufanya. Waongoze kuelewa mawswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi. Majibu watakayotoa yathibitishe kuwa umilisi uliolengwa umefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli Jumlishi**

Kuna mdahalo kati ya wanafunzi wa kidato cha kwanza, **A** na **B.** Wewe utakuwa mmoja wa wasemaji wakuu kutoka darasa la **A** watakaounga mkono mada, "**Wanyama ni muhimu kwa jamii; wanafaa kuhifadhiwa"**

a. Andika hoja utakazotoa kuunga mkono mada ya siku.
b. Unafikiri watakaopinga mada watatoa hoja zipi?
c. Mada ikibadilika na kuwa **"ndege wa porini wana umuhimu mkubwa kwa jamii**" Eleza hoja ambazo utatoa kuunga mkono mada hiyo.
d. Tunga sentensi tano katika wakati uliopo kwa kutumia majina ya wanyama na kisha uzigeuze sentensi hizo kwa wingi.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wamejifunza kuhusu,*

a. majina ya wanyama na ndege wa nyumbani na porini.
b. faida za wanyama na ndege.
c. vikembe mbalimbali.

d. kusoma na kujadili makala yanayohusu sifa za wanyama na ndege.
e. matumizi ya vivumishi vimilikishi katika sentensi.
f. upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya A–WA katika sentensi.
g. kuandika insha ya mwongozo kwa kufasiri michoro kuhusu wanyama na faida zao.

**Jedwali la kutathiminia wanafunzi**.

| **Matarajio** | **Mbinu ya kwanza: Uwiano, Alama 3** | **Mbinu ya pili: Muumano, Alama 3** | **Mbinu ya tatu: Uhakika, Alama 3** | **Mbinu ya nne: Bora zaidi, Alama 1** |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika hoja za kuunga mkono mada | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja sita na zaidi ambazo zinawiana na mada, atuzwe **alama 3/3** **-** Mwanafunzi atakeyeeleza hoja kati ya tatu na tano ambazo zinawiana na mada atuzwe **alama 2/3** **-** Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya moja na mbili ambazo zinawiana na mada atuzwe **alama 1/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zisizowiana na mada aongozwe kurudia kazi/shughuli | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote kwa ufasha zikapata kueleweka vizuri atuzwe alama **3/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya tatu na tano kwa ufasaha, atuzwe **alama 2/3** - Mwanafunzi ambaye ataeleza hoja kati ya moja na mbili kwa ufasaha atuze **alama 1/3** - Mwanafunzi ambaye maelezo yake yatakuwa hayaeleweki kuleta maana, asaidiwe kurudia. | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote ambazo ni sahihi atuzwe **alama 3/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya tatu na tano ambazo ni sahihi atuzwe **alama 2/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja mbili kwenda chini aongozwe kurudia shughuli. | **Hoja moja** ituzwe mwanafunzi ambaye ameonyesha ujuzi wa hali ya juu; kwa mfano, kueleza kwa ufasaha, usahihi au akiwa amejibu maswali ambayo wengine wameshindwa. Mwalimu anaweza kufanya uamuzi wa kutuza hoja hii kutegemea jinsi alivyoona mwanafunzi akitenda. |
| Hoja zitakazotolewa na wale wanaopinga mada | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja 63at una 63at u ambazo zinawiana na mada, atuzwe **alama 3/3** **-** Mwanafunzi atakeyeeleza hoja kati ya 63at una | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote kwa ufasha zikapata kueleweka vizuri atuzwe **alama 3/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya 63at una tano | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote ambazo ni sahihi atuzwe **alama 3/3** - Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya tatu na tano ambazo ni | Hoja moja ituzwe mwanafunzi ambaye ameonyesha ujuzi wa hali ya juu; kwa mfano, kueleza kwa ufasaha, usahihi au akiwa amejibu maswali ambayo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | tano ambazo zinawiana na mada atuzwe **alama 2/3**<br>**-** Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya moja na mbili ambazo zinawiana na mada atuzwe **alama 1/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja zisizowiana na mada aongozwe kurudia kazi/shughuli | kwa ufasaha, atuzwe **alama 2/3**<br>- Mwanafunzi ambaye ataeleza hoja kati ya moja na mbili kwa ufasaha atuze **alama 1/3**<br>- Mwanafunzi ambaye maelezo yake yatakuwa hayaeleweki kuleta maana, asaidiwe kurudia. | sahihi atuzwe **alama 2/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya moja na mbili **alama 1/3**<br>-Aliye chini ya hapo aongozwe kurudia shughuli. | wengine wameshindwa.<br>Mwalimu anaweza kufanya uamuzi wa kutuza hoja hii kutegemea jinsi alivyoona mwanafunzi akitenda. |
| Hoja kuhusu mada ya "ndege wa porini wana umuhimu kwa jamii" | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja sita na zaidi ambazo zinawiana na mada, atuzwe alama **3/3**<br>**-** Mwanafunzi atakeyeeleza hoja kati ya tatu na tano ambazo zinawiana na mada atuzwe alama **2/3**<br>**-** Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya moja na mbili ambazo zinawiana na mada atuzwe alama **1/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja zisizowiana na mada aongozwe kurudia kazi/shughuli | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote kwa ufasha zikapata kueleweka vizuri atuzwe alama **3/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya tatu na tano kwa ufasaha, atuzwe alama **2/3**<br>- Mwanafunzi ambaye ataeleza hoja kati ya moja na mbili kwa ufasaha atuze **alama 1/3**<br>- Mwanafunzi ambaye maelezo yake yatakuwa hayaeleweki kuleta maana, asaidiwe kurudia. | - Mwanafunzi atakayeeleza hoja zote ambazo ni sahihi atuzwe alama **3/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja kati ya tatu na tano ambazo ni sahihi atuzwe alama **2/3**<br>- Mwanafunzi atakayeeleza hoja mbili hadi tatu atuzwe **alama 1/3**<br>-Mwanafunzi atakayekuwa chini ya hapo aongozwe kurudia shughuli. | Hoja moja ituzwe mwanafunzi ambaye ameonyesha ujuzi wa hali ya juu; kwa mfano, kueleza kwa ufasaha, usahihi au akiwa amejibu maswali ambayo wengine wameshindwa.<br>Mwalimu anaweza kufanya uamuzi wa kutuza hoja hii kutegemea jinsi alivyoona mwanafunzi akitenda. |
| Sentensi tano katika wakati uliopo na | Mwanafunzi atakayeandika sentensi zote: | Mwanafunzi atakayeandika sentensi zote katika | Mwanafunzi atakayetunga sentensi kama | Manafunzi atakayejibu kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kuzigeuza zikawa kwa wingi | *Katika wakati uliopo<br>*Kutumia majina ya wanyama<br>*Kuzigeuza kwa wingi<br>Atuzwe alama **3/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayetunga baadhi ya sentensi katika wakati uliopo, baadhi zikageuzwa kwa usahihi na baadhi zikatumia majina ya wanyama, **Alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayekuwa chini ya kiwango cha pili atuzwe **alama 1/3**<br>Yule wa chini yah apo asaidiwe kurudia kazi. | wakati uliopo kwa sahihi, zote akazigeuza kwa wingi kwa usahihi n azote zikawa zinatumia majina ya wanyama. Alama **3/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayetunga baadhi ya sentensi katika wakati uliopo, baadhi zikageuzwa kwa usahihi na baadhi zikatumia majina ya wanyama, **Alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayekuwa chini ya kiwango cha pili atuzwe alama **1/3** na yule wa chini asaidiwe kurudia kazi. | alivyoagizwa zote zikawa sahihi<br>Alama **3/3**<br>Kiwango cha juu ya wastani, atuzwe alama **2**<br>Kiwango cha wastani alama **1** na chini ya wastani, aongozwe kurudia.<br><br>-Mwanafunzi atakayetunga baadhi ya sentensi katika wakati uliopo, akageuza baadhi kwa usahihi na akatumia majina ya wanyama katika baadhi ya sentensi. **Alama 2/3**<br><br>Mwanafunzi atakayekuwa chini ya kiwango cha pili atuzwe alama **1/3** na yule wa chini asaidiwe kurudia kazi. | mtindo ulio bora zaidi<br>Alama **1** |

# MADA KUU 1.5 MIMEA NA MATUNDA





**Misamiati Msingi**

Oksijeni
Takribani
Makaazi
Bakteria
Sayari

**Mada hii itakuwezesha:**

a. kutambua mimea mbalimbali na mazao yake.
b. kubaini misamiati ya matunda na vyakula mbalimbali.
c. kuigiza mazungumzo ya kuagiza chakula hotelini.
d. kusoma na kukariri shairi fupi kuhusu mimea.
e. kutambua matumizi ya upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya KI–VI.
f. kutambua vihusishi na matumizi yake katika sentensi.
g. kueleza vinyume vya vitenzi na kuvitumia katika sentensi.
h. kuandika insha ya mwongozoya mimea mbalimbali kutoka kwa jamii yake.
i. kuandika insha ya mwongozo.

**Utangulizi**

Katika mada hii, wanafunzi watajifunza kuhusu mime ana matunda. Kama mwalimu wao, utawawezesha kutambua na kutumia msamiati unaohusiana na mimea, vyakula na matunda pamoja na vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika mawasiliano. Watatambua umuhimu wa vyakula na matunda kwa afya yao.

**Maandalizi pendekezwa ya mwalimu**

Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Kanda za sauti
- Kadi zenye maadishi ya sauti mbalimbali za Kiswahili
- Chati
- Michoro/picha
- Kanda za video
- Projekta
- Kamusi

**Funzo a. Kutambua mimea mbalimbali na mazao yake**


**Shughuli 1.5 Kusoma na kuandika**

Katika vikundi,

1. Waongoze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa katika makala hii.

Ni wazi kuwa maisha katika uso wa dunia hutegemea ubora wa huduma zitolewazo na mimea pamoja na matunda.

Mimea ni uti wa mgongo wa maisha humu duniani kwa sababu huboresha maisha ya mwanadamu na mazingira.



Kwanza kabisa, kila kitu tunachokila huja moja kwa moja na huku vingine vikiwa si vya moja kwa moja kutoka katika mimea. Tukitazama historia ya mwanadamu, takribani mimea elfu saba, mimea ya aina tofauti tofauti imetumiwa na watu kama chakula. Kando na haya, mimea pia imethibiti mzunguko wa maji. Mimea, husaidia katika usambazaji na usafishaji wa maji yaliyomo katika sayari hii. Mimea huvuta hewa ya kaboni dayoksaidi wakati wa mchana ili kutengeneza chakula na kutuachia

sisi binadamu na wanyama hewa safi ya oksijeni. Bila hewa safi, sisi hatungeweza kuishi. Pia inasaidia katika usafirishaji wa maji kutoka katika udongo hadi kwenye anga. Vile vile, inapaswa tuelewe kuwa robo moja ya madawa yote ambayo sisi hutumia tukiwa wagonjwa hutoka katika mimea. Mbali na haya, watu zaidi ya asilimia sabini hii leo wanategemea mimea kama msingi wa tiba yao. Bila mimea, viumbe wengi kama vile samaki na wanyama wa porini wangekosa makaazi iwapo mimea ingekuwepo. Pia tusihau kuwa mimea huwa ni kama vifaa vya ujenzi ya nyumba zetu.

Kwa upande mwingine, taifa la Uganda limebarikiwa na aina mbalimbali ya matunda kama vile maembe, mapaipai, zeituni, balungi, tikiti maji, nanasi, zambarau, ndimu, zabibu, maparachichi, bibo, tope, ubuyu, ukwaju, tunda nyaya, fenesi, ndizi mbivu, chenza mapera, machungwa mengine mengi.



Si ajabu leo kuwa watu wanaothamini sana matunda wanaishi maisha marefu kuwazidi wale wasiotumia matunda. Matunda huzuia maradhi mwilini na kumfanya mtu awe na afya bora. Hurutubisha mwili na kuupatia kinga. Pia, matunda humpa mwanadamu madini na vitamini mbalimbali zinazosaidia kujenga, kukarabati na hata kuzuia bakteria.

Wanafunzi wamemaliza kusoma Makala hii kwa makini, sasa waongoze kushirikiana katika makundi kutambua na kueleza maana ya maneno mapya kutokana na makala. wanaweza kutumia kamusi.

2. Washirikishe na kuwaongoza kujibu maswali yafuatayo;

i. Taja hoja nne za umuhimu wa mimea katika jamii yako.

Mifano ya majibu ni kama:

- Baadhi ya mime ana matunda ni vyakula vyetu.
- Mimea husaidia kusafisha na kusambaza maji.
- Hutusaidia na hewa safi ya oksijeni
- Baadhi ya mime ana matunda ni dawa kwa binadamu

ii. Watu wanaothamini sana matunda hufikwa na bahati gani?

**Mifano ya majibu ni kama:**

- Huishi Maisha marefu ukiwalinganisha na wale wasiokula matunda.
- Huzuia maradhi na kumfanya mtu kuwa na afya bora.

iii. Je, matunda yana manufaa yoyote katika maisha ya binadamu kulingana na makala uliyosoma hapo juu?

**Mfano wa jibu**: Naam, matunda yana manufaa kwa Maisha ya binadamu. Kwa mfano, humzuia binadamu kushikwa na magonjwa, humpa afya nzuri na kumwezesha kuishi Maisha marefu.

iv. Nenda katika soko lililo karibu na kwenu kisha uandike majina ya matunda unayoyaona.

**Mifano ya majibu watakayoandika ni kama**:

Mananasi, Maembe, Machungwa, Mapaipai, Maparachichi, Mafenesi

**Shughuli 2.5 Kusoma na kuandika**

Wakiwa katika makundi, waongoze wanafunzi,

1. Kusoma na kujadiliana kuhusu mimea na mazao yake kama ifuatavyo.

| **Mmea** | **Zao la Mmea** |
|---|---|
| Mwembe | Embe |
| Mchungwa | Chungwa |
| Mlimau | Limau |
| Mtomoko | Tomoko |
| Mfenesi | Fenesi |
| Mbuyu | Buyu |
| Mpaipai | Paipai |
| Mzabibu | Zabibu |
| Mpera | Pera |
| Mkorosho | Korosho |

2. Washirikishe wanafunzi kutaja mimea sita inayopatikana nyumbani kwao pamoja na mazao yake.

   **Majibu yanayotarajiwa ni kama**: Mpaipai/Mipaipai, Mpera/Mipera, Mbuyu/Mibuyu, Mlimau/Milimau, Mfenesi/Mifenesi

3. Waongoze kusoma na kujadili umuhimu wa mazao mbalimbali ya mimea. Mifano ya majibu watakayotoa ni kama:

- Huwa ni chakula cha binadamu na wanyama.
- Ni mbolea hasa baada ya mazao haya kuozea shambani.
- Ni njia ya ajira ya watu wengine wanaopata kipato chao kwa kuyauza mazao ya mimea.
- Mazao ya mimea huweka kutuletea pesa za kigeni kupitia utalii hasa wakati watalii wanataka kutazama mimea ya kipekee isiyopatikana katika sehemu zingine za ulimwengu.


**Funzo b: Msamiati wa matunda na vyakula mbalimbali.**

**Shughuli 3.5 Kusikiliza na kuzungumza**


Katika vikundi, waongoze wanafunzi,

2. Kutazama na kujadiliana kuhusu majina ya matunda yafuatayo katika Kiswahili.


a


b


c


d


e


f

g  h  i 

| | | |
|---|---|---|
| Maembe | Tikitimaji | Nanasi |
| Chungwa | Parachichi | Fenesi |
| Paipai | Kakara | Mapera |

3. Waongoze kujadiliana kuhusu vyakula vya kawaida kutokana na maeneo wanakotoka na kisha uwashirikishe katika kuwasilisha yale waliokubaliana katika vikundi vyao.
4. Waongoze katika vikundi vyao kujadiliana kuhusu vyakula vifuatavyo:

(a) Maharagwe
(b) Mahindi
(c) Wali
(d) Ngano
(e) Mtama
(f) Mawele

**Funzo c. Kuigiza mazungumzo ya kuagiza chakula hotelini.**

**Shughuli 4.5 Kusikiliza na kuzungumza.**

Katika makundi, waongoze wanafunzi kuigiza mazungumzo yafuatayo:

1. Kwanza, washirikishe katika kusoma na kuigiza mazungumzo ifuatavyo:

**Muhindo:** U hali gani Chepkorir?

**Chepkorir:** Nimepata afueni sasa ingawa bado nahisi maumivu kiasi.

**Muhindo:** Daktari amekuambia nini kuhusu maradhi yanayokusumbua?

**Chepkorir:** Mwenzangu, yangu ni mazito.

**Muhindo:** Mbona sikuelewi?

**Chepkorir:** Daktari aliniambia kuwa ninaugua kutokana na ukosefu wa lishe bora.

**Muhindo:** Kwani wewe huwa huli vizuri?

**Chepkorir:** Sijui, lakini yeye anadhani hivyo.

**Muhindo:** Basi alisema nini hasa?

**Chepkorir:** aliniambia eti mwili wangu una ukosefu wa madini na vitamini.

**Muhindo:** Alaa! Kwa hivyo wewe huwa huli matunda pamoja na mboga za majani.

**Chepkorir:** Ndio. Mimi huwa nikila nyama kwa wingi.

**Muhindo:** Basi hayo ndiyo matatizo. Hakikisha kuwa unapata lishe bora.

**Chepkorir:** Pia daktari ameniambia hivyo.

**Muhindo:** Amekuambia nini hasa kuhusu lishe hili bora?

**Chepkorir:** Ameniambia ninywe maji kwa wingi. Pia ameniambia nile matunda mbalimbali.

**Muhindo:** Basi fanya si ufanye hivyo?

**Chepkoroir:** La, mimi huwa sipendi kula kila matunda na mboga. Kwani nikila mengine huniletea kichefuchefu.

**Muhindo:** Ni yapi haya usiyoyapenda?

**Chepkorir:** Limau, Zabibu chungu, fenesi, tomoko, tikiti maji na pia parachichi.

**Muhindo:** Na yale uyapendayo ni yapi?

**Chepkorir:** Machungwa pekee.

**Muhindo:** Lo! Unafanya makosa makubwa sana rafiki yangu. Nataka uanze kula matunda ya aina mbalimbali ili uwe na afya bora. Mimi unavyoniona huwa nikila matunda na mboga ya aina mbalimbali kila siku ambayo yamenipa afya kama unavyoniona.

**Chepkorir:** Asante kwa ushauri wako mzuri rafiki. Nami nitaanza kula matunda na mboga bila ubaguzi ili niwe na afya nzuri kama yako.

2. Pili, chukua nafasi ya Muhindo huku wao wakiwa Chepkorir na kisha mbadilishane nafasi.
3. Tatu, wajibizane katika vikundi, huku kikundi kimoja kikiwa Muhindo na kingine Chepkorir. Wakimaliza, wabadilishane nafasi.
4. Nne, waweke katika jozi na wazungumze
5. Waongoze kutafuta maneno mapya kutokana na mazungumzo waliyoigiza hapo juu.

**Funzo d: Kusoma na kukariri shairi**

**Shughuli 5.5 Kusikiliza na kuzungumza**

Wanafunzi wakiwa katika makundi,

1. Washirikishe katika kutunga, kusoma, kukariri na kuimba shairi kuhusu mimea. Unaweza kuwaongoza kubuni shairi wao wenyewe au uwape lile ulilotafuta au ulilobuni wewe mwenyewe.

**Sarufi:**

**Funzo e. Kutambua nomino za ngeli ya ki-vi**

**Shughuli 6.5 Kusoma na kuandika**

Katika vikundi, waongoze wanafunzi;

**1.** Kutazama na kujadiliana kuhusu wanachoona katika picha walizopewa.

**Mifano ya sentensi**


a


b


c


d


e


f

**2.** Ambatanisheni maneno au sentensi zifuatazo na picha mlizojadili hapo juu.

| | |
|---|---|
| Hiki ni kitanda | Kisu kile si kikali |
| Kikombe kimevunjika | Kitabu hiki ni kizuri. |
| Chungu chetu ni kizuri | |

**3.** Washirikishe wanafunzi katika kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya nomino katika ngeli ya Ki - Vi

Hii ni ngeli ya nomino ambayo inajumuisha nomino zinazoanza na kiambishi **"Ki**- "kwa umoja na" **Vi**- "kwa wingi. Aidha, kuna baadhi ya nomino katika ngeli hii ambazo huanzia na kiambishi **"Ch-** na **Vy-**" kwa umoja na wingi mfululizo. Kundi hili la "**Ki-Vi/ Ch-Vy**" linajumuisha nomino zisizo na uhai.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kiti | Viti |
| Kikombe | Vikombe |
| Kipara | Vipara |
| Kichana | Vichana |
| Kibuyu | Vibuyu |
| Kioo | Vioo |
| Kisu | Visu |

| | |
|---|---|
| Kijiko | Vijiko |
| Kiazi | Viazi |
| Kifo | Vifo |
| Kiatu | Viatu |
| Choo | Vyoo |
| Chumba | Vyumba |
| Cheti | Vyeti |
| Chandarua | Vyandarua |

**4.** Shirikisha wanafunzi katika vikundi vya watatu watatu kutafuta na kuandika nomino nyingine za ngeli ya Ki-Vi katika umoja na wingi kutokana na kamusi.

**5.** Washirikishe katika kutunga sentensi angalau kumi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya Ki-Vi katika umoja na wingi.

Mifano ya sentensi ambazo utatarajia ni kama:

| Umoja | Wingi |
| --- | --- |
| - Kisu changu hiki ni kikali | Visu vyangu/vyetu hivi ni vikali. |
| - Kikombe cha mtoto kimevunjika | Vikombe vya Watoto vimevunjika. |
| - Chakula chako kimeharibika. | Vyakula vyenu vimeharibika. |

**Funzo f: Kutambua vihusishi mbalimbali**

**Shughuli 7.5 Kusoma na kuandika**

Katika makundi,

1. Shirikisha wanafunzi katika kusoma na kutambua matumizi ya vihusishi mbalimbali.

**Taz:** Vihusishi ni maneno yanayotuarifu zaidi kuhusu uhusiano wa nomino na mazingira yake. Hutuonyesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na jingine. Mifano ya vihusishi ni kama: katika, toka, juu ya, chini ya, na nyuma ya. Mifano Zaidi inafuata.

2. Washirikishe wanafunzi katika kusoma sentensi zifuatazo, kisha wajadiliane kuhusu maana ya sentensi hizo kwa kuongozwa na maneno yaliyopigiwa msitari.

**A**

i. Kuna mpira nyuma ya mti huo.
ii. Anatembea mbele ya gari.
iii. Baba alipumzikia chini ya mti.
iv. Nimesimama juu ya daraja.
v. Watoto wanapenda kuogea kando ya mto.
vi. Embe langu liko karibu na kikapu.
vii. Amekwenda kwa shangazi yake.

3. Washirikishe wanafunzi katika kusoma sentensi zifuatazo, kisha wajadiliane kuhusu maana ya sentensi hizo kwa kuongozwa na maneno yaliyopigiwa msitari.

**B**

i. Ni vizuri kuoga usiku <u>kabla ya</u> kulala.

ii. Mzee alikimbizwa hospitalini <u>baada ya</u> kula paipai lililooza na kugonjeka.

4. Kwa kuongozwa na vihusishi vilivyopigiwa mstari katika **A** na **B**, waongoze wanafunzi kutambua na kutofautisha vihusishi hivyo; kati ya vihusishi vya mahali na vihusishi vya wakati.

5. Waongoze kutunga sentensi moja moja kwa kutumia vihusishi hivi.

(a) Kabla ya
(b) Kando ya
(c) Kwa
(d) Juu ya
(e) Baada ya

6. Waongoze kusoma na kujadiliana kuhusu mifano ifuatayo kisha watunge sentensi moja kwa kila kihusishi.

**a) nyuma ya**
i). Mwizi alijificha nyuma ya nyumba yetu.
ii). Huyu mwanafunzi anapenda kukaa nyuma ya darasa.

**b) hadi/ mpaka**
i). Nimelala tokea jioni hadi asubuhi.
ii). Tulitembea kwa miguu kutoka Chuoni mpaka Kampala.

**ch) toka**
i). Ninatoka mjini sasa.
ii). Baba alitoka kazini saa moja jioni.

**d) bila**
i). Mwanafunzi amekuja shuleni bila vitabu.
ii). Mtoto ametembea bila viatu.

**e) katika**
i). Mwalimu alitwambia kuweka madaftari yetu juu ya meza.

ii). Unalala katika bweni gani?

**f) kwa**

i). Yusufu anakwenda kwa msikiti kusali.

ii). Nimesafiri kwa basi.

**g) tangu/tokea**

i). Nimekuwa Tanzania tokea mwaka wa 2010.

ii). Tumesoma vitabu tangu asubuhi.

**h) na**

i). Mwizi aliingia ndani na bunduki.

ii). SSali aliumwa na mbwa.

**i) miongoni**

i). Isabirye anapenda kuketi miongoni mwa wasichana.

ii). Miongoni mwa walimu mmoja ni kaka yangu.

**j) baada ya**

i). Mwalimu wa Kiswahili atakuja baada ya dakika kumi.

ii). Nitamaliza kazi hii baada ya siku tatu.

7. Washirikishe wanafunzi kutunga angalau sentensi kumi kwa kutumia vihusishi mbalimbali walivyojadili hapo juu. *Rejelea mifano ya sentensi hapo juu*.

**Funzo g: Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia wakati uliopita na ukanushaji wake.**

**Shughuli 8.5 Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi, wakiwa katika vikundi;

1. Kutunga sentensi angalau tano zenye vitendo vinavyofanywa sasa hivi.

   Kwa mfano:

   **Kukubali**

Ndege inatua juu ya mlima.

Matunda yananyewa katika kikombe.

2. Waongoze kukanusha sentensi zao wenyewe kwa kukataa kuonyesha kuwa kitendo hicho hakitendeki.

**Kukanusha/ Kukataa**

Ndege haitui juu ya mlima.

Matunda hayanywewi katika kikombe.

**Funzo h. Kuandika insha**

**Shughuli 9.5 Kuandika**

Wanafunzi wakiwa katika jozi, washirikishe katika kuandika insha fupi kuhusu matunda na mboga wanayoyapenda na wasiyoyapenda huku wakitoa sababu zao. Hakikisha kuwa wanazingatia hatua muhimu na vipengele vya insha.

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. Waongoze kuelewa mawswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi. Majibu watakayotoa yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli Jumlishi**

Nyumbani kwenu, ninyi ni wakulima. Mna mashamba mbalimbali ambamo mnatoa mazao ya mimea mbalimbali. Mimea hii huzaa vyakula mbalimbali pamoja na matunda mbalimbali.

a. Elezea ni mimea ipi mnayolima nyumbani kwenu?
b. Kwa kutaja mazao mbalimbali, simulia jinsi mazao hayo yanavyowafaidi ninyi kama familia nzima.
c. Andika kifungu cha maneno kuhusu taarifa yoyote. Hakikisha kwamba kifungu hiki kina sentensi zenye matumiza ya nomino za ngeli ya ki-vi pamoja na vihusishi.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wamejifunza kuhusu,*

a. Mimea mbalimbali na mazao yake.
b. Misamiati ya matunda na vyakula mbalimbali.
c. Uagizaji wa chakula hotelini.
d. Kukariri shairi fupi kuhusu mimea.

e. Mtumizi ya upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya KI–VI.
f. Vihusishi na matumizi yake katika sentensi.
g. Uandishi wa insha.

Jedwali la kutathiminia wanafunzi

| **Matarajio** | **Mbinu ya kwanza: Uwiano, Alama 3** | **Mbinu ya Pili: Muumano, Alama 3** | **Mbinu ya tatu: Uhakika Alama 3** | **Mbinu ya nne: Bora zaidi Alama 1** |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza mimea wanayolima | -Mwanafunzi atakayeeleza juu ya mimea angalau 7 atuzwe **alama 3/3**<br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya mimea kati ya 4 na 6, atuzwe **alama 2/3**<br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya mimea kati ya miwili na mitatu, **alama 1/3**<br>-Kutoka moja kurudi chini asaidiwe kurudia shughuli. | -Mwanafunzi ambaye ataeleza juu ya mimeakwa ufasha na akauendeleza ufasaha huo atuzwe **alama 3/3**<br>- Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha huo kwa kiasi cha wastani, atuzwe **alama 2/3**<br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini ya wastani, atuzwe **alama 1/3**<br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini sana aongozwe kurudia kazi | -Mwanafunzi atakayetaja na kueleza mimea angalau 7 kwa usahihi, **Alama 3/3**<br>-Mwanafunzi ambaye atataja kati ya mimea 4-6 na kuielezea kwa usahihi, **Alama 2/3**<br>-Mwanafunzi atakayeelezea kati ya mimea 2-3 kwa usahihi, atuzwe **alama 1/3**<br>na yule aliye chini yah apo asaidiwe kurudia kazi. | Mwanafunzi atakayetaja na kueleza juu ya mimea kwa ufasaha na kwa usahihi, atuzwe **alama 1** ya kuwa bora zaidi. |
| Kusimulia jinsi mazao yanavyowafaidi | -Mwanafunzi atakayesimulia hadithi yenye visa vinavyoonyesha jinsi mimea inavyofaidi watu.<br>**Alama 3/3**<br>-Mwanafunzi atakayesimulia visa | -Mwanafunzi ambaye atasimulia visa vyote kwa ufasaha<br>**Alama 3/3**<br>-Atakayesimulia kwa ufasha kwa kiasi ambacho kiko | -Mwanafunzi ambaye amesimulia visa vyote kwa usahihi<br>**Alama 3/3**<br>-Yule ambaye visa vyake sahihi viko wastani, **Alama 2/3** | Mwanafunzi ambaye amesimulia visa vinavyowiana, vinavyoumana na viko sahihi na amevieleza kwa ufasaha |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ambavyo kwa kiasi kikibwa vinawiana na mada, **Alama 2/3**<br>-Mwanafunzi ambaye atasimulia visa ambavyo kwa kiasi kikubwa haviwiani na mada, **Alama 1/3**<br>na<br>-Mwanafunzi atakayesimulia visa ambavyo haviwiani na mada, aongozwe kurudia shughuli. | wastani, **Alama 2/3**<br>-Atakayesimulia visa ambavyo kiasi chake cha ufasaha kiko chini ya wastani, **Alama 1/3**<br>Atakayekuwa chini sana, asaidiwe kurudia kazi. | -Yule ambaye visa vyake sahihi viko chini ya wastani, **Alama 2/3**<br>-Yule ambaye hajatumia visa sahihi<br>**Arudie kazi.** | **Alama 1** |
| Kutunga kifungu cha maneno yaliyotumia vipatanishi vya ngeli ya Ki-Vi | -Mwanafunzi atakayetunga kifungu cha maneno kinacholingana na mada.<br>**Alama 3/3**<br>-Mwanafunzi mwenye kifungu cha maneno kinacholingana na mada kwa kiwango cha wastani,<br>**Alama 2/3**<br>-Mwanafunzi atakayetunga kufungu kinacholingana na mada kwa kiwango kilichoko chini ya wastani,<br>**Alama 1/3**<br>Mwanafunzi atakayekuwa chini yah apo aongozwe kurudia kazi. | -Mwanafunzi atakayetunga kifungu kilichotungwa kwa ufasaha<br>**Alama 3/3**<br>-Mwanafunzi ambaye ufasha wake katika kifungu alichotunga ni wa wastani<br>**Alama 2/3**<br>Mwanafunzi ambaye ufasaha wa kifungu chake uko chini ya wastani, **alama 1/3**<br>Mwanafunzi ambaye ufasaha wake uko chini sana asaidiwe kurudia kazi hiyo. | Mwanafunzi ambaye atatunga kifungu sahihi kwa ujumla<br>**Alama 3/3**<br>Mwanfunzi ambaye ametunga kifungu ambacho usahihi wake uko wastani<br>**Alama 2/3**<br>Mwanafunzi ambaye ametunga kifungu ambacho usahihi wake uko chini ya wastani<br>**Alama 1/3**<br>Yule mwanafunzi ambaye kifungu chake si sahihi asaidiwe kurudia kazi | Mwanafunzi ambaye ametunga kifungu bora kilicho sahihi na fasaha<br>**Alama 1** |

# MADA KUU 1.6: BIASHARA







**Misamiati Msingi**
Sarafu
Salio
Mtaji
Bima
Ununuzi
Uuzaji

Mada hii itakuwezesha:

a. kutambua misamiati ya sarafu mbalimbali.
b. kutambua misamiati ya bidhaa za dukani na sokoni.
c. kabaini misamiati ya ununuzi na uuzaji wa bidhaa.
d. kuigiza mazungumzo ya ununuzi na uuzaji wa bidhaa.
e. kusoma makala yanayohusu shughuli za kibiashara.
f. kutambua matumizi ya upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya I–ZI.
g. kutambua vivumishi vya *a*-unganifu na matumizi yake katika sentensi.
h. kueleza matumizi ya vielezi husika katika sentensi.
i. kuandika insha ya mwongozo ya bajeti kuhusu vile utatumia shilingi 10,000/=.

**Utangulizi**

Katika mada hii, wanafunzi watajifunza kuhusu biashara. Watasoma kuhusu bidhaa mbalimbali na mazingira mbalimbali ambako biashara hufanyiwa. Wewe kama mwalimu, utawaongoza na kuwawezesha kutambua msamiati unaohusiana na biashara na bidhaa mbalimbali.

**Maandalizi pendekezwa ya mwalimu**
Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Kanda za sauti
- Kadi zenye maadishi ya sauti mbalimbali za Kiswahili
- Chati
- Michoro/picha
- Kanda za video
- Projekta
- Kamusi

**Funzo a: Kutambua msamiati wa bidhaa za dukani na sokoni**

**Shughuli 1.6: Kusikiliza na kuzungumza**

Wanafunzi wakiwa katika makundi,

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu msamiati ufuatao na kisha;
   i. waelezee maana ya kila msamiati
   ii. watumie msamiati huo kutunga sentensi kimapokezi

| | | |
|---|---|---|
| chumvi | mtama | mkate |
| kabichi | mawele | mteja |
| sukari | bidhaa | bei |
| mchele | ngano | nyanya |
| wimbi | vibiriti | nyama |

2. (i) Washirikishe katika kutaja bidhaa tano zinazopatikana katika duka lililokaribu na nyumbani kwao. Kwa mfano, vitunguu, nyanya, chumvi, sukari, peremende
   (ii) Waongoze katika kutaja vitu vinavyouzwa katika soko lililoko karibu na kwao, wakitoa mifano. Kwa mfano, wanyama, nguo, vyakula, kuku, viatu

**Funzo b: Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati unaohusiana na ununuzi na uuzaji wa bidhaa**

**Shughuli 2.6: Kusoma na kuandika**

Katika vikundi, waongoze wanafunzi;

i. Kujadili msamiati unaohusiana na ununuzi na uuzaji wa bidhaa na kisha, wautumie msamiati huo kutunga sentensi. Kwa mfano:

- Pesa: Kamusi hii inauzwa pesa ngapi?
- Ghali: Viatu hivi ni ghali sana
- Rahisi: Leo vitu vimekuwa rahisi sikoni.

ii. kusoma kwa usahihi na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati ufuatao:

Pesa Deni Hasara Mtaji Nunua Hisa Bima

Salio Faida Mteja Bidhaa Uza Kipato Bei Fedha

Mifano:

Pesa: Nimetumia pesa nyingi kununua kitabu hiki.

Deni: Agaba hajalipa deni langu la shilingi elfu kumi.

Faida: Biashara isiyo na faida siifanyi mimi.

Mteja: Mteja wangu leo hajaja, sijui kwa nini.

**Funzo c: Kuigiza mazungumzo kati ya mnunuzi na muuzaji**

**Shughuli 3.6: Kusikiliza na kuzungumza**

Wakiwa katika jozi,

Waongoze wanafunzi kuigiza mazungumzo kwa zamu kati ya muuzaji na mnunuzi. Hakikisha kila mzungumzaji azungumze angalau mara sita. Mfano wa mazungumzo:

**Muuzaji:** Karibu mteja wangu, karibu sana. Niko hapa kukuhudumia.

**Mnunuzi:** Asante sana. Leo nimekuja kununua matunda pekee.

**Muuzaji:** Matunda ninayo kwa wingi. Aina zote za matunda unayotaka ninayo.

**Mnunuzi:** Leo ningetaka kununua mananasi, mapera, maparachichi, tikiti maji na maembe.

**Funzo d: Kusoma Makala kuhusu shughuli za kibiashara**

**Shughuli 4.6: Kusoma**

Wakiwa katika vikundi,

i. Waongoze kusoma kimya makala ifuatayo, na kisha wajadiliane ujumbe uliomo katika makala.
ii. Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti makala ifuatayo na kuelezea ujumbe uliomo
iii. Waongoze wanafunzi kujibu maswali yanayopatikana mwishoni mwa makala.

Katika maisha ya binadamu soko ni sehemu nyeti sana ya kibinafsi, kijamii na kitaifa.

Mwanadamu ana mahitaji mengi sana katika kukimu maisha yake na miongoni mwa hayo kubwa ni chakula.

Hatua ya mwanzo imesimamia kilimo na hata wahenga walisema kuwa 'Kilimo ni uti wa mgongo wa maisha'. Kwa maana hiyo bila ya kilimo, maisha ya binadamu yamo mashakani. Pia, bila ya harakati za kilimo, soko halitapatikana kwani bidhaa za sokoni tuzitumiazo zatokana na kilimo. Kwa mfano nguo ni pamba, mbao ni miti na vinginevyo.

Wakulima wengi na wasiokuwa wakulima tegemeo lao kubwa ni soko. Bali si hao tu. Taifa nalo linategemea soko. Mkulima hulima akachukua mazao ya mimea sokoni akauza ili apate fedha. Asiyekuwa mkulima pia shamba lake ni soko na ndio maana wajuzi wa kusema huamba eti soko ni shamba la wavivu. Kwa vile ulimwengu wa siku hizi jinsi ulivyoendelea umetenga maeneo maalum ya kuendesha shughuli kama hizo za uuzaji na ununuaji wa bidhaa za sokoni. Na hapo ndipo pia taifa hupata pato lake kwa kupitia serikali za mitaa kuwatoza ushuru wale washiriki wa biashara zinazofanywa sokoni.

**Maswali**:

Washirikishe wanafunzi kujibu maswali haya kutoka kwa taarifa.

1. Yape makala haya kichwa mwafaka.
   **Jibu tarajiwa**: Soko, Sokoni, Bidhaa za Sokoni
2. Kwa nini soko ni sehemu nyeti sana katika maisha ya binadamu?
   **Jibu tarajiwa**: - Hukimu Maisha ya binadamu kwa kumpa chakula
   - Wakulima huchukua mazao yao sokoni

3. Bidhaa nyingi za sokoni zinatokana na nini?

   **Jibu tarajiwa:** Bidhaa nyingi za sokoni hutokana na kilimo

4 Taja bidhaa zinazotokana na ukilima/ kilimo.

   **Jibu tarajiwa:** Mbao, Nguo, vyakula, n.k

5 Ni nini tegemeo kubwa la wakulima?

   **Jibu tarajiwa:** Ni soko

**Sarufi**

**Funzo e: Kutambua nomino za ngeli ya i-zi na kuzitumia kutunga sentensi kwa kuzingatia vipatanishi vya ngeli ya i-zi**

**Shughuli 5.6: Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi katika vikundi,

1. kutambua nomino za ngeli ya i-zi kwa umoja na wingi na kisha kila mwanafunzi aziandike katika daftari lake.
   Mifano ya nomino ni kama:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Nguo | Nguo |
| Bidhaa | Bidhaa |
| Nyumba | Nyumba |

2. kutunga sentensi sahihi kwa kutumia nomino za ngeli ya i-zi kwa umoja na wingi.
   Mifano ya sentensi ni kama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Nguo hii inapendeza. | Nguo hizi zinapendeza. |
| Bidhaa hii ni rahisi | Bidhaa hizi ni rahisi. |
| Nyumba hii itatumiwa kesho | Nyumba hizi zitatumiwa kesho. |

**Funzo f: Kutunga sentensi kwa kutumia nyakati mahsusi**

**Shughuli 6.6: Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na Kuandika**

Katika vikundi, mwalimu awaongoze;

Kumbushana msamiati wa biashara ulioko katika ngeli ya i-zi na kuutumia kutunga sentensi sahihi. Sentensi zitungwe kwa umoja na wingi kwa kutumia njeo zifuatazo: **na, ta, li, me**.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Njeo ya -na-** | |
| Nguo hii inapendeza sana. | Nguo hizi zinapendeza sana. |
| Bidhaa hii inauzwa pesa nyingi. | Bidhaa hizi zinauzwa pesa nyingi. |
| **Njeo ya -ta-** | |
| Hasara ambayo amepata ni kubwa. | Hasara ambazo wamepata ni kubwa. |
| Sahani hii itauzwa pesa nyingi. | Sahani hizi zitauzwa pesa nyingi. |
| Kalamu hii itatumiwa na wanafunzi. | Kalamu hizi zitatumiwa na wanafunzi. |
| **Njeo ya -li-** | |
| Pesa zangu za kununua kamusi ziliibwa. | Pesa zetu za kununua kamusi zillibwa. |
| Pamba yako iliuzwa pesa nyingi. | Pamba zenu ziliuzwa pesa nyingi. |
| **Njeo ya -me-** | |
| Nguo hii imependwa na wengi. | Nguo hizi zimependwa na wengi. |
| Simu yangu imeharibika sana. | Simu zetu zimeharibika sana. |

**Funzo g: Kuandika insha juu ya bajeti ya shilingi 10,000 utakazotumia**

**Shughuli 7.6: Kuandika**

Katika vikundi, waongoze wanafunzi;

Kujadiliana kuhusu jinsi watakavyotumia shilingi elfu kumi. Baada ya majadiliano, watunge insha juu bajeti ya shilingi elfu kumi au kiasi chochote cha pesa. Insha ya kila kikundi iwekwe kwenye chati na kutundikwa ukutani ili wanavikundi vingine waione.

Waongoze kupitia vijenzi vya insha nzuri wakizingatia:

- Kichwa
- Mwili
- Tamati
- Idadi ya maneno

Pia wazingatie sarufi, tahajia ya maneno, uakifishaji, mbinu nyingine za Sanaa.

***Taz:*** Sarafu ni vipande vya fedha, karatasi au shaba vinavyothaminiwa na kutumiwa kama pesa za nchi husika.

| **Sarafu** | **Taifa/nchi** |
|---|---|
| Shilingi | Uganda/ Kenya/ Tanzania |
| Dola | Marekani |
| Pauni | Uingereza |
| Faranga | Ufaransa/ Ubelgiji/ Rwanda, n. k |
| Dinari | Nchi za Mashariki ya kati |












**Shughuli ya Jumla**

Wazazi wako wamekupa shilingi 50,000 kwenda kununua vitu kutoka sokoni. Vitu utakavyonunua ni vya kutumia wakati wa sherehe ya kuzaliwa kwa dada yako ambako kutakuwako wiki ijayo.

a. Taja majina ya vitu ambavyo utanunua ili kuvitumia katika sherehe hiyo.
b. Kwa kila kitu ulichonunua, tumia jina la kitu hicho kutunga sentensi kwa umoja na wingi.
c. Simulia hadithi kuhusu jinsi ulivyotoka nyumbani kwenda sokoni, vitu ulivyonunua na namna ulivyorudi nyumbani.
d. Chagua Rafiki yako humo darasani na muigize mazungumzo; wewe ni mnunuzi na yeye ni muuzaji.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, umejifunza kuhusu*

a. kutambua misamiati ya sarafu mbalimbali.
b. kutambua misamiati ya bidhaa za dukani na sokoni.
c. kabaini misamiati ya ununuzi na uuzaji wa bidhaa.
d. kuigiza mazungumzo ya ununuzi na uuzaji wa bidhaa.
e. kusoma makala yanayohusu shughuli za kibiashara.

f. kutambua matumizi ya upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya I–ZI.
g. kutambua vivumishi vya *a*-unganifu na matumizi yake katika sentensi.
h. kueleza matumizi ya vielezi husika katika sentensi.
i. kuandika insha ya mwongozo ya bajeti kuhusu vile utatumia shilingi 10,000/=.

**Utathimini wa shughuli jumlishi**

Zingatia:

Fuata mfano wa utathimini wa shughuli jumlishi za hapo awali ili kutathimini wanafunzi katika shughuli jumlishi hii.

# MUHULA WA TATU

# MADA KUU: 1.7 NYUMBA



**Misamiati Msingi**
Sebule
Maakuli
Makochi
Uwastani
Faragha
Dohani
Runinga
Vimelea

Mada hii itakuwezesha:

a. kutambua na kutaja sehemu za nyumba.
b. kuimba wimbo na kueleza ujumbe wake.
c. kuelewa vitu vinavyopatika katika sehemu mbalimbali za nyumba.
d. kujadili umuhimu wa vitu katika nyumba.
e. kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
f. kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya **U–Zi** katika sentensi.
g. kubainisha matumizi ya vivumishi viashiria/vionyeshi katika sentensi.
h. kuweza kuamrisha na kutekeleza amri na ukanushi wake.
i. kutambua kiambishi cha wakati uliopona matumizi yake katika sentensi.
j. kutambua hatua mwafaka za uandishi wa insha.

**Utangulizi**

Katika mada hii, wanafunzi watajifunza kuhusu sehemu za nyumba. Pia watajifunza kuhusu umuhimu wa kila sehemu ya nyumba. Waongoze wanafunzi kutaja aina za nyumba, sehemu za nyumba na vitu vinavyopatikana katika nyumba.

Kwa hivyo mada hii itampa mwanafunzi uwezo wa kutambua aina za nyumba, sehemu za nyumba mbali mbali pamoja na vitu vinavyopatikana katika nyumba.

**Mandalizi pendekezwa ya Mwalimu**

Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Vitu halisi
- Michoro
- Picha
- Chati
- Projekta
- Kanda za video

**Funzo a: Kutambua sehemu za nyumba**

**Shughuli 1.7: Kusikiliza, kuzungumza na kuandika**

1. Katika funzo hili, waongoze wanafunzi kujadiliana juu ya sehemu za nyumba. Kwa mfano, sebule, sakafu, chumba cha kulala, jikoni, bafu, choo,
2. Waongoze kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao mbele ya darasa.
3. Waongoze kuandika majina ya vitu vinavyopatikana katika nyumba.
4. Waongoze kuchora na uhakikishe kwamba wanachora michoro mizuri ya nyumba zenye sehemu mbalimbali.

**Funzo b: Kuimba wimbo kuhusu vitu vinavyopatikana katika nyumba**

**Shughuli 2.7: Kusikiliza na kuzungumza**

1. Waongoze wanafunzi katika vikundi vyao kubuni na kuimba wimbo kuhusu vitu vinavyopatikana katika nyumba.
2. Waongoze wanafunzi kueleza ujumbe uliomo katika wimbo wao.

**Funzo c: Kutaja vitu vinavyopatikana katika sehemu mbalimbali za nyumba**

**Shughuli 3.7: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**,

1. Washirikishe wanafunzi kujadiliana na kuandika vitu vinavyopatikana katika sehemu mbalimbali za nyumba kwa mfano; shuuka, magododoro, viti, koki, meza vitanda, pazia nk
2. Kila kikundi kitaje vitu hivyo ili vikundi vingine vilinganishe na vile vya kikundi kilichowasilisha.

**Funzo d: Kujadili umuhimu wa vitu vinavyopatikana katika nyumba**

**Shughuli 4.7: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu vitu vinavyopatikana katika nyumba.
2. Kila kikundi kieleze kuhusu umuhimu wa vitu vinavyopatikana katika Nyumba huku Mwalimu akiwakosoa.

**Funzo e: Kusoma Makala**

**Shughuli 5.7: Kusoma**

1. Waongoze wanafunzi katika kusoma makala ifuatayo kwa makini wakiwa kimya na kutambua ujumbe uliomo.
2. Washirikishe kujadiliana kuhusu ujumbe uliomo katika Makala.
3. Waongoze tena kusoma makala ifuatayo kwa sauti na kisha wajibu maswali yanayofuata.

Nyumba ni jengo ambalo huwa likitumiwa kama makaazi ya binadamu. Nyumbani ni muhimu sana kwa sababu humhifadhi mtu wakati wowote anapohitaji uhifadhi hasa wakati wa usiku ambapo nje huwa na hatari yake.

Hapo kale, mababu zetu waliishi katika nyumba zao zilizokuwa zikiitwa **mapango** ambayo yalikuwa na vijisehemu vingi sana. Hata hivyo, siku hizi mambo yamebadilika kwa sababu maisha ya kale ya kuishi mapangoni yamepitwa na wakati. Katika enzi za leo, nyumba za kisasa zimeenea katika sehemu mbalimbali humu nchini.

Nyumba hizi zinaweza kugawanywa katika makundi tofauti tofauti. Kuna zile za ghorofa na zisizo za ghorofa. Hali kadhalika, kuna nyumba zilizojengwa kwa kutumia udongo ambazo hufahamika kama nyumba za muda na zile zilizojengwa kwa kutumia saruji ambazo ni za

kudumu. Watu wasio na uwezo wa kumiliki nyumba za ghorofa wala za saruji huamua kujenga nyumba za udongo.

Nyumba ya **uwastani** huwa na sehemu mbalimbali ndani yake. Kwanza kabisa tuna sebule. Hiki ni chumba cha kuwakaribisha wageni. Vile vile, ni mahali ambapo mikutano na mazungunzo yasiyo ya **faragha** hufanyikia ndani ya nyumba. Katika sebule vitu ambavyo hupatikana mle ni pamoja na viti vya kulalia, meza, mkeka, saa ya ukutani, redio, **runinga,** kabati, feni na kadhalika.



Sebule

Jikoni nayo ni sehemu nyingine muhimu ndani ya nyumba ambapo chakula hupikiwa. Sehemu hii imejengwa kiufundi sana kwa sababu huwa na **dohani,** ambayo ni tundu linalopitisha moshi. Hata hivyo, sio kila nyumba huwa na jikoni ndani yake. Kuna wale watu ambao jikoni zao huwa nje ya nyumba kuu kwa sababu wao hupika kwa kutumia kuni. Vitu kama vile visu, vijiko, uma, sufuria, sahani, bakuli, sinia na kadhalika hupatikana jikoni.



Jikoni la kisasa



Jikoni la kitamaduni

Choo ni sehemu nyingine muhimu katika nyumba. Kuna choo cha maji ambacho huwa kiko ndani ya nyumba na kile kisicho cha maji ambacho huwa kiko nje. Zaidi ya haya, choo kisichotumia maji, ambacho ni cha kitamadun, kinafaa kiwe ni cha urefu wa mita thelathini kutoka kwa nyumba kuu ili kuepukaa na maradhi yanayoweza kujitokeza kutokana na **vimelea** vinavyosambazwa na nzi wachafu.



Choo cha maji



Choo kisicho cha maji

Chumba cha kulala pia hupatikana ndani ya nyumba. Hapa ni mahali ambapo watu hupumzikia baada ya shughuli zao za mchaka kutwa. Katika chumba cha kulala, vitu vinavyopatikana mle ndani ni pamoja na kitanda, shuka, godoro, mto, blanketi na kadhalika.



Chumba cha kulala

**Maswali**

(a) Jikoni la kisasa na la kitamaduni, ni lipi unalopenda? Toa sababu.

(b) Tazama kwa makini mchoro wa sehemu ya sebule na utaje vitu unavyoona.


(c) Tumia kamusi kueleza maana ya maneno yaliyokolezwa.

**Sarufi**


**Funzo f: Kutunga sentensi sahihi kwa kuzingatia vipatanishi vya kisarufi vya ngeli ya U-Zi**

**Shughuli 6.7: Kusoma na kuandika**

1. Washirikishe wanafunzi kujadiliana kuhusu nomino za ngeli ya u-zi na kuzitaja kwa umoja na wingi.
2. Wanafunzi washirikiane katika kutunga sentensi sahihi huku wakizingatia nomino za ngeli ya u-zi.
3. Wanafunzi watunge sentensi ishirini zenye vivumishi viashiria; kumi zikiwa kwa umoja na kumi zikiwa kwa wingi.
4. Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zifuatazo kwa sauti na kwa usahihi.




Hu**u** ni ukuta



Hi**zi** ni kuta



Uso huu ni mzuri




Nyuso hizi ni nzuri



Ufunguo ule si mkubwa



Funguo zile si kubwa



Uzi huu ni wangu



Nyuzi hizi ni zangu



Ufagio ule unapendeza



Fagio zile zinapendeza

**Taz:** Ngeli hii hujumuisha nomino zinazowakilishwa na **U-** katika umoja na **ZI-** katika wingi, kwa mfano,

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ukuta **u**mebomoka | Kuta **zi**mebomoka |
| Uzi **u**mekatika | Kuta **zi**mekatika |
| Uso **u**naonekana vizuri | Nyuso **zi**naonekana vizuri |

**Funzo g: Kutoa na kutekeleza amri**

**Shughuli 7.7: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

1. waigizeni wanafunzi vitendo vya kutoa na kuitikia amri kwa umoja na wingi.
2. Wanafunzi wabadilishane nafasi ili aliyetoa amri kwanza, sasa aitikie amri.

**Funzo h: Kutambua na kutekeleza hatua mwafaka za kuandika insha**

**Shughuli 8.7: Kusoma na kuandika**

1. Washirikishe wanafunzi kujadiliana kuhusu hatua mwafaka za kuandika insha nzuri.
2. Wanafunzi katika makundi yao wafafanue hatua walizojadili.

**Funzo i: Kuandika insha**

**Shughuli 9.7: Kuandika**

1. Waongoze kujadiliana juu ya sehemu za nyumba.
2. Waongoze wanafunzi katika makundi kuandika insha juu ya sehemu za nyumba na Insha iwe kati ya maneno 150-200

**Zingatia;**

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. waongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi. Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli Jumlishi**

Umemaliza masomo yako na umehitimu na shahada ya kwanza, na sasa umepata kazi. Kwa sababu hiyo, umepata pesa kutoka kwa kazi ambayo unafanya na sasa unataka kujenga nyumba.

(i) Tambulisha aina za nyumba ambazo umewahi kuona.
(ii) Eleza sehemu za nyumba ambazo ungependa nyumba yako iwe nazo.
(iii) Taja vitu ambavyo vinafaa kuwa katika nyumba.
(iv) Ungekuwa na wafanyakazi wakikujengea nyumba, igiza jinsi utakavyokuwa unaamrisha wafanyakazi wako ambao watakujengea nyumba.
(v) Eleza sababu angalau tano kwa nini nyumba ya kisasa ni bora kuliko ya kitamaduni.

**Muhtasari wa Mada**

***Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu***:

a. Sehemu za nyumba na umuhimu wake.
b. Kuimba wimbo na kueleza ujumbe uliomo.
c. Vitu vinavyopatika katika sehemu mbalimbali za nyumba.
d. Kujadili umuhimu wa vitu katika nyumba.
e. Kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
f. Upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya **U–Zi** katika sentensi.
g. Kubainisha matumizi ya vivumishi viashiria/vionyeshi katika sentensi.
h. Kuamrisha na kutekeleza amri na ukanushi wake.
i. Viambishi vya wakati katika sentensi.
j. Hatua mwafaka za uandishi wa insha.
k. Kuandika insha ya mwongozo.

**Jedwali la kutathiminia wanafunzi**

| **Matarajio** | Mbinu ya kwanza: **Uwiano,** Alama 3 | Mbinu ya Pili**:** **Muumano,** Alama 3 | Mbinu ya tatu: **Uhakika** Alama 3 | Mbinu ya nne: **Bora zaidi** Alama 1 |
|---|---|---|---|---|
| Tambua aina za nyumba ambazo umewahi kuona. | -Mwanafunzi atakayetoa aina za nyumba angalau 6 apewe **alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya aina za nyumba kati ya 4 na 6, atuzwe **alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya aina za nyumba kati ya mbili na tatu, **alama 1/3**<br><br>-Kutoka moja kurudi chini asaidiwe kurudia shughuli. | -Mwanafunzi ambaye ataeleza juu ya aina za nyumba kwa ufasaha na akauendeleza ufasaha huo atuzwe **alama 3/3**<br><br>- Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha huo kwa kiasi cha wastani, atuzwe **alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini ya wastani, atuzwe **alama 1/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini sana aongozwe kurudia kazi | -Mwanafunzi atakayetaja na kueleza aina za nyumba angalau 6 kwa usahihi, **Alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi ambaye atataja kati ya aina za nyumba 4-6 na kuzieleza kwa usahihi, **Alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeelezea kati ya aina za nyumba kati ya 2-3 kwa usahihi, atuzwe **alama 1/3** na yule aliye chini ya hapo asaidiwe kurudia kazi. | Mwanafunzi atakayetaja na kueleza juu ya aina za nyumba kwa ufasaha na kwa usahihi, atuzwe **alama 1** ya kuwa bora zaidi. |
| Eleza sehemu za nyumba ambazo ungependa nyumba yako iwe nazo kisha utaje vitu ambavyo vinafaa kuwa | -Mwanafunzi atakayeelezea sehemu zote msingi za nyumba na vitu angalau 6 ambavyo vinafaa kuwa katika nyumba. **Alama 3/3** | -Mwanafunzi ambaye ataelezea sehemu zote za nyuma kwa ufasaha na pia akaorodhesha vitu muhimu vinavyopatikana katika nyumba **Alama 3/3** | -Mwanafunzi ambaye ataelezea sehemu zote za nyumba kwa usahihi na vitu ambavyo vinafaa kuwa katka nyumba **Alama 3/3** | Mwanafunzi ambaye ataelezea kwa ufasaha akizingatia uwiano, muumano wa mambo, **Alama 1** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| katika nyumba. | -Mwanafunzi atakayeelezea sehemu za nyumba kati ya 3-4 na baadhi ya vitu mbalimbali vipatikanavyo katika nyuma **Alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi ambaye ataelezea sehemu za nyumba na vitu vile ambavyo vinafaa kuwa katika nyumba lakini kwa kiasi kikubwa haviwiani na mada, **Alama 1/3**<br>na<br>-Mwanafunzi atakayelezea sehemu za nyumba na vitu ambavyo haviwiani na mada, aongozwe kurudia shughuli. | -mwanafunzi atakayeelezea sehemu za nyumba kwa ufasha na vitu vinavyofaa kuwa katika nyumba kwa kiasi ambacho kiko wastani, **Alama 2/3**<br><br>-Atakayeelezea sehemu za nyumba pamoja na vitu vipatikanavyo katika nyumba na mealezo yake yako chini ya wastani, **Alama 1/3**<br><br>Atakayekuwa chini sana, asaidiwe kurudia kazi. | -Yule ambaye maelezo yake ni sahihi na yako wastani, **Alama 2/3**<br><br>-Yule ambaye maelezo yake sahihi yako chini ya wastani, **Alama 2/3**<br><br>-Yule ambaye hajatoa sehemu za nyumba na vitu sahihi **Arudie kazi.** | |
| Ungekuwa na wafanyakazi wakikujengea nyumba, igiza jinsi utakavyokuwa unaamrisha wafanyakazi wako ambao watakujengea nyumba. | -Mwanafunzi ambaye ataigiza vizuri namna atakayeamrisha wafanyi kazi wake **Alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeigiza kwa kiwango cha wastani, **Alama 2/3** | -Mwanafunzi atakayeigiza kwa ufasaha **Alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi ambaye ufasha wake katika kuigiza mada yake ni wa wastani **Alama 2/3**<br><br>Mwanafunzi ambaye ufasaha | Mwanafunzi ambaye ataigiza kwa usahihi kila kitu **Atuzwe 3/3**<br><br>Mwanfunzi ambaye ameigiza na usahihi wake uko wastani **Alama 2/3**<br><br>Mwanafunzi ambaye ataigiza na | Mwanafunzi ambaye ameigiza kwa usahihi na ufasaha **Alama 1** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | -Mwanafunzi atakayeigiza na ya kuamrisha wafanyi kazi wake kwa kiwango kilichoko chini ya wastani, **Alama 1/3**<br><br>Mwanafunzi atakayekuwa chini ya hapo aongozwe kurudia kazi. | wa kuigiza uko chini ya wastani, **alama 1/3**<br><br>Mwanafunzi ambaye ufasaha wake uko chini sana asaidiwe kurudia kazi hiyo. | usahihi wake uko chini ya wastani **Alama 1/3**<br>Mwanafunzi ambaye maigizo yake sio sahihi asaidiwe kurudia kazi | |
| Eleza sababu angalau tano kwa nini nyumba ya kisasa ni bora kuliko ya kitamaduni. | -Mwanafunzi atakayetoa sababu angalau 6 apewe **alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya sababu kati ya 4 na 6, atuzwe **alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeeleza juu ya sababu kati ya mbili na tatu, **alama 1/3**<br><br>-Kutoka moja kurudi chini asaidiwe kurudia shughuli. | -Mwanafunzi ambaye ataeleza juu ya sababu kwa ufasaha na akauendeleza ufasaha huo atuzwe **alama 3/3**<br><br>- Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha huo kwa kiasi cha wastani, atuzwe **alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini ya wastani, atuzwe **alama 1/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeuendeleza ufasaha kwa kiasi cha chini sana aongozwe kurudia kazi | -Mwanafunzi atakayetaja na kueleza sababu angalau 6 kwa usahihi, **Alama 3/3**<br><br>-Mwanafunzi ambaye atataja sababu kati ya 4-6 kwa nini nyumba ya kisasa ni bora kuliko ya kitamaduni na kuzieleza kwa usahihi, **Alama 2/3**<br><br>-Mwanafunzi atakayeelezea sababu kati ya 2-3 kwa usahihi, atuzwe **alama 1/3**<br>na yule aliye chini ya hapo asaidiwe kurudia kazi. | Mwanafunzi atakayetaja na kueleza juu ya sababu kwa ufasaha na kwa usahihi, atuzwe **alama 1** ya kuwa bora zaidi. |

# MADA KUU 1.8 SHULENI



**Misamiati Msingi**
Nyanja
Kushinikizwa
Maamuzi
Ubabe dume
Kuzini
Dhalilisha
Nyanja
Shahaha
Stashahada

Mada hii itakuwezesha;

a. kutambua watu wa shuleni.
b. kueleza kazi za watu wa shuleni.
c. kuheshimu watu wanaofanya kazi shuleni.
d. kuthamini sehemu watu shuleni wanakofanyia kazi.
e. kubaini vitu vya shuleni.
f. kueleza matumizi ya vitu vya shuleni.
g. kutambua vizuizi dhidi ya maamuzi ya busara.
h. kutambua umuhimu wa habari sahihi kuhusu maamuzi bora.
i. kutambua athari ya maamuzi mabaya maishani.
j. kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
k. kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya U–YAkatika sentensi.
l. atambue kauli za mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yake katika sentensi.
m. atambue kiambishi cha wakati uliopita pamoja na matumizi yake katika sentensi.
n. abaini kiambishi kanushi cha wakati uliopita na akanushe sentensi.
o. atambue hatua mwafaka za uandishi wa insha ya mwongozo.

## Utangulizi

Katika mada hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu umuhimu wa elimu kwa binadamu kama haki ya msingi. Atajifunza pia kutambua na kutumia misamiati unaohusiana na shuleni pamoja na vipengele vya lugha vilivyoteuliwa katika mawasiliano.

**Mandalizi pendekezwa ya Mwalimu**

Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Vitu halisi
- Michoro
- Picha
- Chati
- Projekta
- Kanda za video

**Funzo a. Kutambua Watu shuleni**

**Shughuli 1.8 Kusikiliza na kuzungumza**

Washirikishe kujadiliana na kutaja watu mbalimbali wanaopatikana katika shule zao.

**Funzo b. Kueleza kazi za watu wa shuleni**
**Shughuli 2.8 Kusoma na kuandika**

2. Wanafunzi washirikiane na wenzao kujadiliana kuhusu kazi mbalimbali za watu wa shuleni huku wakiongozwa na Mwalimu.
3. Waambatanisha watu wa shuleni wafuatao na wajibu wake.

| Mtumishi | Wajibu wake |
|---|---|
| Mwalimu wa nidhamu Naibu wa | Anamsaidia Mwalimu Mkuu kuendesha majukumu yake |
| Mhasibu | Anasimamia shughuli za masomo shuleni. |
| Mwalimu Mkuu. | Anasimamia shughuli zote shuleni. |
| Mwalimu Mkuu. | Huhakikisha kuwa nidhamu imedumishwa shuleni miongoni mwa wanafunzi. |
| Msimamizi wa Masomo | Husimamia hesabu za matumizi ya pesa. |
| Askari | Husimamia usalama wa shuleni. |
| Mhazili | Huwapikia wanafunzi na walimu chakula. |
| Mshauri na mwongozi. | Huwashauri na kuwaongoza wanafunzi |
| Muuguzi | Huwatibu wanafunzi. |
| Mpishi | Kuhifadhi nyaraka za shule. |

**Funzo c. Kutambua sehemu watu wanakofanyia kazi shuleni**

**Shughuli 3.8 Kusikiliza na kuzungumza**

1. Wanafunzi wataje na kujadili sehemu mbalimbali ambako watu wa shuleni hufanyia kazi zao.
2. Kwa kutumia mifano, waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu tabia zinakubalika katika sehemu ambazo watu hufanyia kazi.
3. Washirikishe wanafunzi kujadiliana kuhusu wanachojua juu ya sehemu mbalimbali zifuatazo.

| | | |
|---|---|---|
| Ofisi | Jikoni | Uani |
| Maabara | Zahanati | Msalani |
| Lango kuu | Maktaba | Ghala |

**Funzo e. Kubainisha umuhimu wa vitu vya shuleni**

**Shughuli 4.8 Kusoma na kuandika**

1. Wanafunzi wajadiliane na wenzao kuhusu umuhimu mbalimbali wa vitu vya shuleni.
2. Washirikishe wanafunzi kusoma na kisha waandike kuhusu umuhimu wa vitu vya vinavyopatikana shuleni.

Vitu ambavyo hupatikana shuleni huwa na umuhimu mkubwa sana kwa walimu, wanafunzi pamoja na wafanyikazi wote waliomo. Kwa mfano;

Darasa - huwa likitumiwa kuwafunzia wanafunzi.

Ofisi ya Mwalimu mkuu - huwa ikiwakaribisha na kuwashughulikia wageni.

Kengele - Huwa inawafahamisha wanafunzi na walimu kuhusu mwisho wa vipindi inapopigwa.

Chaki - kifaa kinachotumiwa kuandikia ubaoni.

Ubao - mwalimu hukitumia kwa kuandika juu yake ili wanafunzi watazame.

Chati - hutumiwa kuonyesha maandishi au michoro kwa maelezo ya ziada.

Kalamu - ni kifaa cha wanafunzi na walimu cha kuandikia vitabuni.

Kitabu - hutumiwa katika kubeba matini inayoandikwa kwa kalamu.

3. Waongoze wanafunzi kutaja na kujadiliana kuhusu vitu vinavyotumika sana shuleni kwao.

**Funzo f. Kusoma makala**

**Shughuli 5.8 Kusoma na kuandika**

1. Wanafunzi washirikiana kuandika na kusoma makala fupi kuhusu watu wa shuleni
2. Waongoze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu makala ifuatayo na kisha wajibu maswali.

**Kufanya maamuzi ya busara**

Maamuzi ya busara huwa yana faida kubwa sana katika maisha ya mhusika. Wanafunzi wanafaa kuwa na mwelekeo mwema katika maisha yao ambayo itaongozwa na aina ya maamuzi wanayoyafanya.

Hata hivyo, imekuwa ni vigumu kwa wanafunzi na watu wengine kufanya maamuzi ya busara kutokana na vizuizi vifuatavyo:

- Tabia za kujiunga na makundi mabaya ya wanafunzi.
- Tamaa ya pesa ambapo mwanafunzi anajikuta mtegoni.
- Maisha ya kuzini.
- Ushauri mbaya kutoka kwa marafiki wa karibu.
- Ubabe dume katika jamii unaomdhalilisha mtoto wa kike.
- Wazazi wasiojali maisha ya wanao.

**<u>Umuhimu wa maamuzi ya busara</u>**

Habari sahihi kuhusu maamuzi ya busara ni muhimu kwa sababu;

- Inamfanya mwanafunzi ajiheshimu na kutofanya maamuzi mabaya maishani.
- Mwanafunzi anaweza kutulia darasani na kufanya vyema katika mitihani yake.
- Inamwepusha mwanafunzi dhidi ya maovu yanayoweza kumletea madhara.

**<u>Athari za maamuzi mabaya shuleni na nyumbani</u>**

Athari za maamuzi mabaya shuleni na nyumbani ni pamoja na;

- Vifo vya mapema kwa waathiriwa.
- Kuanguka mitihani shuleni.
- Kuambukizwa maradhi ya zinaa.
- Kufukuzwa shuleni kwa mwanafunzi.
- Kunajisiwa.

**SHUGHULI ZA SHULENI**

1. Washirikishe wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa ifuatayo;

Shule huwa na shughuli mbalimbali. Kando na masomo ambapo wanafunzi hutarajiwa kufundishwa na walimu wao, kuna mambo mengine ambayo hufanyika pia. Shughuli hizi ni kama zifuatazo:

Michezo – Katika nyanja hii wanafunzi huhusika katika mashindano mbalimbali ikiwemo kandanda, riadha, kuogelea, mpira wa vikapu, mpira wa mikono na mengineyo.

Vilabu na vyama – Kuna pia vilabu mbalimbali ambavyo huwashirikisha wanafunzi tofauti tofauti. Hata hivyo, mwanafunzi hujiunga katika vilabu na vyama hivi kwa hiari yake mwenyewe bila kushinikizwa. Vilabu na vyama hivi ni pamoja na vile vya; Maskauti, Msalaba mwekundu, Drama na Uigizaji, Midahalo, Utunzaji misitu, uandishi wa habari na vingine vingi.

3. Wanafunzi washirikiane na wenzao katika makundi kujibu maswali yafuatayo;

(a) Taja shughuli za shuleni zilizozungumziwa katika taarifa hii.
(b) Unadhani vyama vya Maskauti na Msalaba Mwekundu vina umuhimu gani shuleni?
(c) Ni shughuli zipi ambazo hazijazungumziwa katika taarifa hii lakini ungependa ziwemo katika shule yako?

**Tanbihi; Msamiati wa ziada shuleni**

1. Wanafunzi washirikiane na wenzao katika makundi na wajadiliane kuhusu msamiati zaidi wa shuleni ufuatao;

Mada, kidato/darasa, mtihani, maabara, maktaba, kalamu, daftari, bweni, ubao, ratiba, chaki, kamusi, karatasi, ukumbi wa shule, shamba la shule, shule ya bweni, shule ya kutwa, kanisa la shule, msikiti wa shule, ua la shule, jiko la shule, chumba cha walimu, cheti cha stashahada, shahada, muhula, likizo, michezo, stakabadhi, n.k.

Wanafunzi wajajadiliane na wenzao katika kujibu maswali yafuatayo;

a. Toa manufaa mawili ya:

i. Maabara

ii. Maktaba

iii. Bweni

iv. Ukumbi wa shule

b. Tunga sentensi tano ukitumia haya maneno:

a) Kidato

b) Mtihani

c) Ubao

d) Mwanafunzi

e) Mchezo

**Sarufi:**

**Funzo g. Kutunga sentensi kwa kutumia nomino za Ngeli ya ‘‘U-YA’’**

**Shughuli 6.8. Kusoma na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana na wenzao kuhusu matumizi ya nomino za ngeli ya **U**-**Ya**
2. Wanafunzi watunge sentensi sahihi na mwalimu asahihishe na kutoa marekebisho.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii huanza kwa kiambishi **‘‘U**-’’ kwa umoja na **‘‘Ma-**’’ kwa wingi

**Mifano,**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ugonjwa | Magonjwa |
| Ugomvi | Magomvi |
| Ulaji | Malaji |
| Uovu | Maovu |
| Uamuzi | Maamuzi |
| Upishi | Mapishi |

3. Waongoze wanafunzi Katika makundi madogo kusoma na kujadiliana kuhusu maana ya sentensi zifuatazo;

i. Ugonjwa huu ni hatari
ii. Uovu wao ni mbaya
iii. Ugomvi wetu umeisha

iv. Upishi wake si mbaya
v. Ulaji wako ni wa kimaskini.

i. Magonjwa haya ni hatari
ii. Maovu yao ni mabaya
iii. Magomvi yetu yameisha
iv. Mapishi yake si mabaya
v. Malaji yako ni ya kimaskini.

4. Wanafunzi washirikiane na wenzao katika kusoma sentensi zifuatazo na kisha waziandike upya katika umoja.

(i) Wacha maovu yako.
(ii) Watu maskini wana malaji mabaya**.**
(iii) Maamuzi yetu ni sahihi.
(iv) Tumechoka magomvi yenu ya kila siku.
(v) Magonjwa haya yameenea kila mahali.

**Funzo h. Kutumia kauli mbalimbali za Mnyambuliko wa vitenzi**
**Shughuli 7.8 Kusoma na kuandika**

1. waongoze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu kauli mbalimbali za vitenzi zifuatazo;

**(Kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa)**

- Mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitenzi vinavyobadilika kulingana na kauli/hali mbalimbali.

 **Kauli ya Kutenda** - Kitendo katika hali yake ya kawaida (bila kunyambuliwa)

 **Kauli ya Kutendea** - Kufanya kitendo kwa niaba (au kwa ajili) ya mtu mwengine

 **Kauli ya Kutendwa** - Kuathirika moja kwa moja na kitendo.

2. Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu mabadiliko ya vitenzi katika jedwali lifuatalo.

| **Kauli ya kutenda** | **Kauli ya kutendea** | **Kauli ya kutendwa** |
|---|---|---|
| Fanya | Fanyia | Fanywa |
| lima | Limia | Limwa |
| pika | Pikia | Pikwa |
| Lia | Lilia | ? |

| | | |
|---|---|---|
| *Ku*la | Lia | Liwa |
| Penda | Pendea | Pendwa |
| Omba | Ombea | Ombwa |
| Tembea | Tembelea | Tembelewa |
| Abudu | Abudia | Abudiwa |

3. Wanafunzi washirikiane na wenzao katika vikundi kunyambua vitenzi hivi katika kauli waliyopewa mabanoni:

i. Anguka (kauli ya kutendea)
ii. Fundisha (kauli ya kutendwa)
iii. Kimbia (kauli ya kutendwa)
iv. Okoa (kauli ya kutendea)
v. Somwa (Kauli ya kutenda)

4. Washirikishe wanafunzi katika kutunga sentensi zao wenyewe angalau tano na wabadilishe kila sentensi katika kauli walizopewa.

**Funzo i. Kutambua na kutumia kiambishi cha wakati uliopita - li –**

**Shughuli 8.8 Kusoma na kuandika**

1. Waongoze wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu wanachotazama katika jedwali.

| **Kiwakilishi** | **alama ya wakati** | **Kitenzi** | **kielezi/ yambwa** |
|---|---|---|---|
| Ni- | -li- | Soma | kitabu |
| A- | - li- | Cheza | kandanda |
| U- | - li- | Leta | maji |
| M- | -li- | Andika | barua |
| Tu- | -li- | Fanya | mtihani |
| Wa- | -li- | Enda | shuleni |

2. Washirikishe wanafunzi katika kutunga sentensi zao wenyewe huku wakiongozwa na mifano katika jedwali lililojuu.
3. Waongoze wanafunzi tena kusoma mifano ifuatayo na kisha watunge sentensi katika njeo nyingine yoyote wanayojua.

1. Mwalimu a**li**fundisha juzi.

2. Baba a**li**nunua gari mwaka jana.

3. Ni**li**andika barua asubuhi.

4. A**li**soma Kiswahili

5.Tu**li**cheza kandanda vizuri

**Zingatia:** Wakati uliopita huonesha kitendo ambacho kilifanyika katika majira yaliyopita/ muda mrefu uliopita.

**i. Mtindo wa kukubali**

Tazama jedwali lifuatalo;

4. Wanafunzi washirikiana katika kusoma kwa sauti sentensi zifuatazo.

Soma sentensi hizi kwa sauti.

1. Nilisoma kitabu.
2. Alicheza kandanda.
3. Ulileta maji.
4. Mliandika barua.
5. Tulifanya mtihani.
6. Walienda shuleni.

**ii. Mtindo wa kukanusha**

Katika hali ya kukanusha, viwakilishi vinageuzwa hadi mtindo wa kukanusha, alama ya wakati ambayo ni **–li-** inageuka –ku-. Kwa mfano,

a) Ni**li**soma barua. - Si**ku**soma barua.

4. washirikishe wanafunzi Katika jozi kusoma kwa sauti na kujadiliana kuhusu sentensi zifuatazo zilizokanushwa.

(a) Hakucheza kandanda.
(b) Hukuleta maji.
(c) Hamkuandika barua.
(d) Hatukufanya mtihani.
(e) Hawakuenda shuleni.

**Zingatia:** Vitenzi vya silabi moja katika hali ya kukanusha hupoteza **ku-**.

Kwa mfano;

1. Sikula chakula jana.
2. Hakuja nyumbani.
3. Hatukunywa maji.
4. Wagonjwa hawakufa.

5. Musa hakuwa rais wetu.

6. Wanafunzi washirikiane na majirani yao darasani katika kukanusha sentensi hizi zifuatazo.

1. Mama alisahau kupika chakula.
2. Tulizungumza Kiswahili.
3. Waliezeka nyumba.
4. Baguma alitandika kitanda chake.
5. Kanzira alicheza muziki na Mutesi.
6. Kato alikuja shuleni jana.

**Funzo j. Kuandika Insha**

**Shughuli 9.8 Kuandika**

Waongoze wanafunzi katika makundi kuandika insha inayoanza; "Siku yangu ya kwanza katika shule ya upili ilikuwa ya kusisimua..."

**Zingatia;**

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. waongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi. Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli jumlishi**

Tangu ujiunge na shule yako hii, umepata marafiki ambao mshazoeana. Mnashirikiana katika kufanya kazi mbalimbali shuleni, Shuleni pia, kuna watu mbalimbali ambao hushughulikia kazi mbalimbali shuleni.

a. Kwa maelezo, simulia jina lako, shule yako, inapatikana wapi? ni kitu gani unapenda kuhusu shule yako? Ni watu wanaopatikana shuneni kwako? Watu hao wanasaidia katika kufanya zipi? Ni sehemu zipi za shuleni unazojua na ni shughuli zipi zinazotendeka huko?
b. Yaandike masimulizi yako uliyoyatoa hapo juu.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu,*

a. Watu wa shuleni.

b. Kzi za watu wa shuleni.
c. Watu wanaofanya kazi shuleni.
d. Vitu vya shuleni.
e. Matumizi ya vitu vya shuleni.
f. kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
g. Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U–YAkatika sentensi.
h. Kauli za mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yake katika sentensi.
i. Kiambishi cha wakati uliopita pamoja na matumizi yake katika sentensi.
j. Ukanushaji wa kiambishi kanushi cha wakati uliopita na akanushe sentensi.
k. Uandishi wa insha

Zingatia:

Fuata mfano wa utathimini wa shughuli jumlishi ya hapo awali ili kutathimini wanafunzi katika shughuli jumlishi hii.

# MADA KUU 1.9: MICHEZO



**Misamiati Msingi**
Mkakamavu
Udhaifu
Anufaike
Kukadirika
Nadra
Kisaikolojia
Masibu
Waliowakwasi
Maarufu

Mada hii itakuwezesha:

a. kutambua na kutaja michezo mbalimbali.
b. kuwataja wachezaji mashuhuri wa nchini na kimataifa.
c. kucheza michezo.
d. kubainisha vifaa vya michezo.
e. kutaja manufaa ya michezo.
f. kuelewa namna ya kuepukana na ajali katika michezo.
g. kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
h. kutambua upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya U–I katika sentensi.
i. kubainisha matumizi ya viunganishi.
j. kutunga sentensi kwa kuzingatia wakati timilifu.
k. kukanusha sentensi za wakati timilifu.
l. kutambua hatua za uandishi wa insha.
m. kuandika insha ya mwongozo.

**Utangulizi**

- Katika mada hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu michezo na manufaa yake kwa nchi mbalimbali. Pia atajifunza kuhusu aina za michezo na vifaa vinavyotumiwa katika michezo mbalimbali. vilevile wanafunzi watajifunza namna wataweza kujikinga kutokana kwa ajali wakiwa wanacheza. Mada hii itawahimiza wanafunzi kushiriki katika michezo ili kufurahia manufaa yao.

**Mandalizi pendekezwa ya Mwalimu**

Katika mada hii, unaweza kuandaa au kutumia vifaa vifuatavyo;

- Vitu halisi kama mipira, Kamba, gori nk
- Michoro
- Picha
- Chati
- Kanda za video

**Funzo a: Kutaja michezo mbalimbali inayochezwa**

**Shughuli 1.9: Kusikiliza na kuzungumza**

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana juu ya michezo mbalimbali inayochezwa na kisha kila kikundi kitaje michezo kiliyojadili mbele ya darasa.
2. Washirikishe wanafunzi katika kuigiza michezo inayohusisha mbio namna inavyochezwa.
3. Waongoze wanafunzi kusoma na kuigiza jinsi michezo mbalimbali inavyochezwa.

1. Mieleka: Ni mchezo ambao watu wawili hushindana nguvu kwa kupigana na kuangushana au kubiringishana.

3. Mpira wa vikapu: Ni mchezo wa mpira ambao timu mbili hushindana katika kutupa mpira kwa mikono kuuingiza katika kikapu kinachokuwa juu.

4. Voliboli - Mchezo wa timu ya watu sita unaochezwa kwa mikono kwa kupiga mpira na kuuvusha juu ya wavu ulioweka katikati ya kiwanja kuelekea timu pinzani.

5. Mpira wa pete/netiboli - Mchezo wa mpira wa mikono unaochezwa na watu saba kila upande kwenye uwanja ambao goli zake ni milingoti miwili mirefu yenye pete na nyavu.

6. Hoki - Mchezo wa mpira ambao wachezaji hucheza kwa kutumia magongo maalumu.

7. Gofu - Mchezo unaochezwa kwa kuupiga mpira mdogo kwa kingoe.

8. Naga/gori - Mchezo unaofanana na mpira wa mguu ambao wachezaji huruhusiwa kukamata mpira na kukimbia nao.

9. Chesi/saratanji/bao - Mchezo unaofanana na bao ambao huchezwa na watu wawili ambapo kila mmoja anakuwa na vipande 6 vya kucheza vinavyoweza kusogezwa juu ya ubao wenye umbo mraba kwa uelekeo tofauti.

10. Kareti - Mtindo wa upiganaji wa kijapani ambapo mpiganaji hutumia mikono na miguu.

11. Judo - Mchezo wa mieleka ambao huchezwa na watu wawiliwawili.

12. Kriketi - Mchezo unaochezwa na timu mbili ambapo kila moja inakuwa na mchezaji.

13. Mbio - mwendo wa kasi au upesi.

14. Jugwe - Mchezo wa kuvutana kwa kamba unaochezwana timu mbili zenye wachezaji kumi na wawili kila moja.

15. Msabaka - Mashindano ya mbio za farasi wanaoongozwa na wapanda farasi.

16. Sarakasi - Michezo inayofanywa kwa ustadi mkubwa ambayo huonyesha matendo ya kishujaa na ya kushangaza.

17. Mlenge - Mashidano ya kulenga shabaha kwa kutupa vijiti vinane.

18. Langalanga - Mbio za vijigari vidogo dogo.

19. Kuogelea: Mchezo wa kuogelea majini.

**Funzo b: Kujadili michezo na wachezaji mashuhuri wa kimataifa**

**Shughuli 2.9 Kusikiliza, kusoma na kuandika**

1. Wanafuninzi watazameni picha zifuatazo na waelezee wanachoona kutokana na picha hizo.
2. Washirikishe wanafunzi kuambatanisha msamiati wa michezo waliousoma hapo awali na picha hizi.




a




b




c



d



e



f



e



f



g

1. Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu michezo na wachezaji mashuhuri wa kimataifa na kisha katika makundi:
   a. Wanafunzi wataje wachezaji mashuhuri ambao wanajua.
   b. Wanafunzi wataje michezo ambayo wachezaji hao hucheza.
   c. Wanafunzi wataje na kuigiza jinsi michezo hiyo inavyochezwa.
2. **Washirikishe wanafunzi Jadiliana kujibu maswali yafuatayo;**

i. Mchezo wa kushikana na kuangushana huitwa _____.
ii. Jina jingine la mchezo wa soka ni mchezo wa _____.
iii. Mchezo wa ngumi pia huitwa _____.
iv. Mchezo wa soka huwa na wachezaji wangapi kila upande?
v. Mchezo wa kuruka kwa kutumia mti huitwa?
vi. Mchezo wa watoto wa kugotanisha miguu miwili pamoja na kurukaruka kwa kwenda mbele na nyuma ni _____.
vii. Mchezo wa kuvuta kamba wa timu za watu kumi na wawili kila upande huitwa _____.
viii. Mashindano ya mbio za farasi au watu ni _____.
ix. Mchezo wa magongo uchezwao na watu wawili au wanne ambao huingiza mipira katika vishimo huitwa _____.
x. Mbio za vijigari vidogo huitwaje? _________ .

**Taz:** 1. Soka/kandanda/kambumbu ni mchezo unaochezwa kwa miguu na huchezwa na timu mbili zinazoshindana.

3. Wanafunzi wasome na kujadiliana kuhusu wachezaji wafuatao

**Mchezo wa tenisi** **Wachezaji mashuhuri wa michezo mbalimbali**

| | **Jina la mchezaji** | **Aina ya mchezo** | **Uraia** |
|---|---|---|---|
| 1. | Stephen Kiprotich | Mbio za masafa marefu | Mwana Uganda |
| 2. | Geoffrey Massa | Kandanda | Mwana Uganda |
| 3. | Dorcus Inzikuru | Mbio za masafa marefu | MwanaUganda |
| 4. | Serena Williams | Tenisi | Mmarekani |
| 5. | Michael Jordan | Mpira wa vikapu | Mmarekani |
| 6. | John Mugabi | Masumbwi | Mwana Uganda |
| 7. | Michael Schumacher | Magari ya langalanga | Mjerumani |
| 8. | Sarah Sjostrom | Uogeleaji | Mswidi |
| 9. | Sam Ssali | Mbio za magari | Mwana Uganda |
| 10. | Peace Proscovia Drajole | netiboli | Mwana Uganda |

4. Waongoze wanafunzi kutazama na kusoma jedwali la wachezaji mashuhuri.
5. Washirikishe wanafunzi kutaja wachezaji mashuhuri unaowajua wewe pamoja na michezo yao.

**Funzo c: Kubainisha vifaa vinavyotumiwa katika michezo**

**Shughuli 3.9: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

Wanafunzi wajadiliana kuhusu vifaa ambavyo hutumiwa katika michezo na kisha:

a. Wanafunzi katika vikundi wachore vifaa walivyovitambua
b. Wanafunzi katika vikundi tena wadhihirishe jinsi kila kifaa hutumiwa.
c. Washirikishe wanafunzi pia kujadiliana kuhusu mwonekano na matumizi ya vifaa vifuatayo;

| | | |
|---|---|---|
| Kamba | Firimbi | Wanyama |
| Mpira | Boti | Viatu maalum |
| Mbao telezi | Baiskeli | Magongo |
| Maleba ya kuogelea | Pikipiki | |

**Funzo d: Kutengeneza vifaa vya kutumia katika michezo**

**Shughuli 4.9: Kusikiliza na kuzungumza**

Kwa kushirikiana katika jozi;

a. Waongoze wanafunzi katika kutengeneza vifaa vya kutumia katika michezo.
b. Washirikishe wanafunzi wasimame mbele ya darasa na kuelezea namna vifaa hivyo vinavyotengenezwa.

**Funzo e: Kueleza manufaa ya michezo**

**Shughuli 5.9: Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika**

Waongoze wanafunzi kujadiliana juu ya michezo mbalimbali na kisha;

a. Watambue manufaa ya michezo kwa jamii fulani na nchi kwa ujumla.
b. waeleze manufaa ya michezo waliyojadili katika vikundi vyao.
c. wajadiliane na kusoma kuhusu manufaa ya michezo yafuatayo;

i. Huchangamsha ubongo ili ufanye kazi vizuri.

ii. Huleta afya bora
iii. Huzuia maradhi kumshambulia mtu kwa urahisi.
iv. Michezo humfanya mtu kuwa mwenye furaha kila wakati.
v. Michezo ni ajira kwa watu wengine.
vi. Inakuza ushirikiano na umoja watu wanapokuja pamoja kutazama michezo.
vii. Inaletea nchi sifa hasa wachezaji mashuhuri wanapotamba.

**Funzo f. Namna ya kuepukana na ajali katika michezo.**

**Shughuli 6.9 Kusikiliza na kuzungumza**

Wakiwa katika vikundi, waongoze wanfunzi;

1. kujadiliana kuhusu wachezaji na michezo wanayocheza
2. watambue jinsi wachezaji wanavyoweza kujikinga dhidi ya ajali mbali mbali katika michezo.
3. kusoma na kujadiliana mambo muhimu yafuatayo;

i. Epukana na kufanya mambo kwa harakaharaka bila mpango.
ii. Kanuni za mkufunzi lazima zifuatwe kwa makini sana.
iii. Vaa mavazi yanayopaswa kushabihina na aina ya mchezo husika.
iv. Epukana na ulaji wa vyakula vingi sana wakati wa michezo.
v. Mazoezi ya muda kwa muda yanapaswa kufanya ii viungo vya mwili viwe sawa.
vi. Iwapo mtu anahisi dalili zote za maumivu, amwone daktari mara moja.

**Funzo g. Ufahamu**

**Shughuli 7.9 Kusoma na kuandika**

Katika makundi, waongoze wanafunzi;

1. kusoma na kujadiliana kuhusu taarifa katika Makala hii.

Michezo ina faida nyingi katika katika maisha ya binadamu. Kuna aina nyingi sana ya michezo katika jamii kama vile kandanda, mpira wa pete, riadha, masumbwi na kadhalika.

Ukiwa kama mwana michezo ndani ya jamii kwanza unakuwa na afya ya kutosha katika mwili wako kutokana na mazoezi ambayo huwa unafanya mara kwa mara. Basi utakuwa mkakamavu na afya tele.

Pili, kama mwana michezo, mtu yeyote anayefanya mazoezi ni vigumu sana kupata maradhi ya mara kwa mara kutokana na mazoezi anayoyafanya. Vijidudu vingi vya maradhi

humshambulia mtu ambaye ana udhaifu katika mwili wake. Kwa wale wanaofanya mazoezi, tatizo hili huwa ni nadra sana kuwapata.

Vile vile, mchezaji kila wakati huwa ni mwenye furaha. Hii ni kwa sababu michezo huwa ikimfanya mtu kupata utulivu wa kisaikolojia na hivyo basi kusahau masaibu ambayo yamekuwa yakimwandama. Ni asilimia ndogo sana ya wana michezo ambao hawana raha ikilinganishwa na wale ambao wana raha.

Michezo ni ajira. Baadhi ya wanamichezo humu duniani wamefanya michezo kuwa kazi zao kwa sababu ya malipo mazuri wanayoyapata kutokana na michezo hiyo. Kuna baadhi ya wana michezo waliowakwasi sana kwa kutokana na michezo kiwango cha kuwashtua hata viongozi maarufu wa kisiasa ulimwenguni.

Kupitia michezo, tunafunzwa kutumia mawazo na akili zetu kwa sababu katika mchezo wowote ule, lazima mchezaji awe mbunifu ndio aweze kushinda. Bila kuwaza kimaantiki, mchezaji anaweza kugonga mwamba, na hiyo iwe ndiyo mwisho wa ndoto yake maishani.

Katika hitimisho hivyo basi, michezo ina faida nyingi sana ambayo haiwezi kukadirika. Ni wajibu wa kila mtu, mdogo kwa mkubwa, awe mpenzi wa michezo ili anufaike zaidi katika maisha yake.

2. Washirikishe wanafunzi katika kusoma na kujibu maswali yanayofuata.

i. Je, habari hii inastahili kuwa na mada ya aina gani? Pendekeza.
ii. Dondoa mifano mitatu ya michezo iliyozungumziwa katika ufahamu huu.
iii. Mtu ambaye ana udhaifu katika mwili wake hupatwa na shida gani kulingana na mwandishi?
iv. Ni ushauri upi anaotoa mwandishi katika aya ya mwisho?
v. Je, habari hii inakufunza nini?

**Sarufi**

**Funzo h: Kutumia nomino za ngeli ya u-i**

**Shughuli 8.9 Kusoma na kuandika**

Katika makundi, waongoze wanafunzi;

1. Kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya nomino za ngeli ya u-i katika sentensi.

**Ngeli ya U-I**

Ngeli hii hurejelewa kama ngeli ya U-I kwa sababu nomino katika ngeli hii huwakilishwa na '**U'** katika umoja na **'I'** katika wingi. Nomino katika ngeli hii huanza na **'M'** katika umoja na **'MI'** katika wingi. Katika ngeli hii, kuna majina ya mimea, miti na nomino nyingine.

Washirikishe wanafunzi kusoma na kujadiliana kuhusu mifano ya nomino za ngeli hii.



Mhogo



Mihogo



Mgomba



Migomba




Mhindi



Mihindi



Mwembe



Miembe



Mpaipai



Mipaipai




Mnazi



Minazi



Mkate




Mikate




Mfuko



Mifuko



Mkono



Mikono



Mguu




Miguu




Mshipi



Mishipi



Msikiti



Misikiti

**Mifano ya sentensi za umoja katika ngeli ya U-I**

1. Mkate huu ni mtamu.
2. Mfuko wangu ni mkubwa.
3. Mpapai ule si mrefu.
4. Mguu wake umevunjika.

**Mifano ya sentensi za wingi katika ngeli ya U-I**

1. Mikate hii ni mitamu.
2. Mifuko yangu si mikubwa.
3. Mipapai ile si mirefu.
4. Miguu yangu imevunjika.

2. Washirikishe wanafunzi katika vikundi vyao kutunga sentensi sahihi katika umoja na wingi kwa kutumia nomino zifuatazo.

(a) Mkebe
(b) Mfereji
(c) Mlima
(d) Mpini
(e) Mkufu

## Funzo i. Kutumia Viunganishi katika utunzi wa sentensi

### Shughuli 9.9. Kusoma na kuandika

Katika makundi, washirikishe wanafunzi;

1. kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya viunganishi katika utunzi wa sentensi.

**Zingatia.** Viunganishi ni maneno yanaoyotumiwa kuunganisha neno moja na lingine, fungu la maneno na lingine au sentensi na nyingine.

**Mifano ya viunganishi;**

1. **kama**
   i) Utapata kazi kama utasoma Kiswahili.
   ii) Mpishi atapika chakula kama atapata kuni.
2. **kwa hiyo/hivyo**
   i) Sijapata pesa nyingi kwa hiyo sitanunua gari.
   ii). Hatujalipa karo kwa hiyo hatutaenda shuleni.
3. **pia**
   i) Wazazi pia watazungumza Kiswahili.
   ii) Mimi pia nilimwona rais.

4. **kwa sababu**
   i) Sikusoma jana kwa sababu nilikuwa mgonjwa.
   ii) Hakupita mitihani kwa sababu hakusoma kwa bidii.
5. **lakini**
   i) Nilienda shuleni lakini sikumwona mwalimu mkuu.
   ii) Nguruwe huyu anakula lakini hashibi.
6. **ingawa**
   i). Ingawa inanyesha, nitaenda shuleni.
   ii). Nitajibu swali hili ingawa ni gumu.
7. **kisha**
   i) Mbabazi alichukua ng`ombe malishoni kwanza kisha akaenda shuleni.

ii) Wanafunzi watasafisha darasa kwanza kisha waingie wasome

8. **au/ ama**
   i) Unataka kalamu au kitabu.
   ii) Ama nitakula wali au ugali.
9. **ili**
   i) Nimekuja shuleni ili nione mwalimu wa Kiswahili.
   ii) Tumesoma Kiswahili ili tupate kazi.
10. **ila/isipokuwa**
   i) Wanafunzi wote waingie darasani ila Okello.
   ii) Watu wote watalipa isipokuwa wanafunzi.

2. Washirikishe wanafunzi katika kusoma na kuunganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi sahihi.

i. Wananchi wanapenda amani. Wananchi wanapenda usawa.
ii. Mwalimu huyu atafundisha. Atapata chaki.
iii. Nipe kalamu. Nipe karatasi.
iv. Nilitaka kumsaidia. Sikuwa na uwezo.
v. Mtu huyu anatumia pesa ovyo. Ni mwizi.

3. Waongoze kujadiliana na kutunga angalau sentensi mbili kwa kila kiunganishi kutokana na vifuatavyo.

(a) Pia
(b) Ilhali
(c) Isipokuwa
(d) Licha ya
(e) kwamba

**Funzo j. Kutunga sentensi katika - hali timilifu -me-**

**Shughuli 10.9 Kusoma na kuandika**

Katika makundi, waongoze wanafunzi;

1. Kusoma na kujadiliana kuhusu matumizi ya hali timilifu.

Hali hii inatumiwa kuonesha kuwa kitendo kimetimika kabla ya kutolewa kwa taarifa.

**Kwa mfano;**
**Soma sentensi hizi kwa sauti.**

1. Nimechota maji.
2. Mohamed amekula ugali.
3. Rais ameteua mawaziri.

4. Kafeero ameenda Kampala
5. Nimekamilisha zoezi.

| Mtindo wa kukubali | Mtindo wa kukanusha |
|---|---|
| Nimepiga kelele. | Sijapiga kelele. |
| Amepika chakula. | Hajapika chakula. |
| Umesafisha vyombo. | Hujasafisha vyombo. |
| Mmekuja hapa. | Hamjaja hapa. |
| Tumefanya kazi. | Hatujafanya kazi. |
| Wamekunywa pombe. | Hawajanywa pombe |

## Tanbihi:

Katika mtindo wa kukanusha, alama ya wakati-**me** hugeuka –**ja**-. Vitenzi vya silabi moja, hupoteza –**ku**- ya vitenzi jina katika hali ya kukanusha.

**2. Shirikiana katika makundi kujibu maswali yafuatayo**

a. Andika sentensi hizi katika hali ya kukanusha

i. Baba amekuja shuleni
ii. Mwalimu amefundusha leo.
iii. Leo tumekula chakula.
iv. Nimepata fedha zangu.
v. Wanafunzi wamepita mitihani yao.

**Funzo k. Kuandika Insha**

**Shughuli 11. 9 Kuandika**

Katika makundi, washirikishe wanafunzi kuandika insha kuhusu mchezo mpendao na kisha mwasilishe kazi yenu kwa wenzenu darasani.

**Zingatia;**

Katika shughuli jumlishi ifuatayo, hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa wanachoagizwa kufanya. waongoze kuelewa maswali yaliyomo na kila mwanafunzi ayajibu kibinafsi. Majibu watakayotoa, yathibitishe kuwa matarajio yaliyolengwa yamefikiwa na kutimizwa.

**Shughuli jumlishi**

Shuleni kwenu kuna michezo mbalimbali. Wanafunzi mblimbali hupenda kucheza michezo mbalimbali pia. Kuna televisheni ambako siku za wikiendi, wanafunzi hutazamia michezo mbalimbali ya kitaifa na ya kimataifa.

a. Elezea kuhusu michezo mbalimbali inayochezwa shuleni, jinsi inavyochezwa, vifaa vinavyotumiwa katika michezo hiyo.
b. Kwa nini unafikiri ni muhimu kushiriki katika michezo mbalimbali ya wanafunzi.

**Muhtasari wa mada**

*Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu;*

a. Michezo mbalimbali.
b. Wachezaji mashuhuri wa nchini na kimataifa.
c. Vifaa vya michezo mbalimbali vya michezo
d. Manufaa ya michezo.
e. Jinsi ya kuepukana na ajali katika michezo.
f. Kusoma na kujibu maswali kutokana na makala.
g. Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U–I katika sentensi.
h. Matumizi ya viunganishi.
i. Utunzi wa sentensi kwa kuzingatia wakati timilifu.
j. Ukanushaji wa sentensi za hali timilifu.
k. Hatua za uandishi wa insha.
l. Uandishi wa insha.

Zingatia:

Fuata mfano wa utathimini wa shughuli jumlishi ya hapo awali ili kutathimini wanafunzi katika shughuli jumlishi hii.

NCDC
NATIONAL CURRICULUM
DEVELOPMENT CENTRE

National Curriculum
Development Centre,
P.O. Box 7002, Kampala.
www.ncdc.go.ug